



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

**HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII MHESHIMIWA  
DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA (MB) WAKATI AKIWASILISHA  
BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA  
MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

**Dodoma**

**Mei, 2018**

## YALIYOMO

YALIYOMO.....	i
1.0 UTANGULIZI.....	1
2.0 DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA .....	3
3.0 UMUHIMU WA MALIASILI, MALIKALE NA UTALII.....	4
3.1. Maeneo ya Maliasili na Malikale .....	4
3.2. Mchango wa Maliasili, Malikale na Utalii katika Mazingira na Uchumi.....	5
4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII.....	7
5.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 .....	8
5.1 Ukusanyaji Maduhuli.....	8
5.2 Matumizi ya Kawaida na Maendeleo.....	9
5.3 Mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni .....	9
5.4 Majukumu ya Wizara na Taasisi zake.....	10
5.4.1. Sekta Ndogo ya Wanyamapori .....	10
5.4.2 Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki.....	22
5.4.3 Sekta Ndogo ya Utalii .....	30
5.4.4 Sekta Ndogo ya Malikale.....	35
5.4.5 Miradi ya Maendeleo.....	40
5.5 Masuala Mtambuka.....	44
5.5.1. Utawala na Raslimaliwatu .....	44
5.5.2. Kuanzisha Jeshi Usu .....	44
5.5.3. Mifumo na Matumizi ya TEHAMA.....	45
5.5.4. Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa .....	45
5.5.5. Utatuzi wa Migogoro .....	46
5.6 Majukumu ya Kimkakati.....	47
5.6.1. Kutekeleza Agizo la Serikali la kuhamia Dodoma.....	47
5.6.2. Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Rufiji.....	47

5.6.3.	Kuwezesha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji kwenye Sekta.....	47
5.7	Mafanikio, Changamoto na Utatuzi Wake.....	48
5.7.1	Mafanikio.....	48
5.7.2	Changamoto .....	48
5.7.3	Utatuzi wa Changamoto .....	50
6.0	MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 .....	50
6.1.	Ukusanyaji Maduhuli.....	50
6.2.	Matumizi ya Kawaida na Maendeleo.....	51
6.3.	Mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni .....	51
6.4.	Kazi Zitakazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake .....	51
6.4.1.	Sekta Ndogo ya Wanyamapori .....	51
6.4.2.	Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki.....	55
6.4.3.	Sekta Ndogo ya Utalii .....	59
6.4.4.	Sekta Ndogo ya Mambo ya Kale .....	60
6.5.	Miradi ya Maendeleo.....	62
6.6.	Masuala Mtambuka.....	63
6.6.1.	Utawala na Raslimaliwatu .....	63
6.6.2.	Kuanzisha Jeshi Usu .....	63
6.6.3.	Mifumo na Matumizi ya TEHAMA.....	63
6.6.4.	Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa .....	64
6.6.5.	Kutatua Migogoro.....	64
6.6.6.	Majukumu ya Kimkakati.....	64
7.0	SHUKRANI.....	64
8.0	MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 .....	65
9.0	HITIMISHO.....	65
	VIAMBATISHO .....	66

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1:	Makusanyo ya Maduhuli ya Idara, Taasisi na Mifuko ya Wizara kwa Mwaka 2016/2017, Makisio na Makusanyo hadi Machi 2018, na Makadirio kwa Mwaka 2018/2019.....	66
Jedwali Na. 2:	Makusanyo ya Maduhuli ya Mashirika ya Wizara kwa mwaka 2016/2017, Makisio na Makusanyo hadi Machi 2018, na Makadirio kwa mwaka 2018/2019.....	67
Jedwali Na. 3:	Mgawanyo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida (Halisi) kwa Idara, Vitengo na Taasisi za Wizara kwa Mwaka 2016/2017, Bajeti na Matumizi hadi Machi 2018 na Makisio kwa Mwaka 2018/2019 .....	68
Jedwali Na. 4:	Makadirio ya Matumizi kwa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2018/2019...	69
Jedwali Na. 5:	Idadi ya Watalii wa Ndani na Nje Waliotembelea Hifadhi za Taifa na Mapato yaliyopatikana kuanzia 2013/2014 hadi Machi 2018.....	71
Jedwali Na. 6:	Idadi ya Watalii wa Ndani na Nje Waliotembelea Mamlaka ya Ngorongoro na Mapato yaliyopatikana kuanzia 2013/2014 hadi Machi, 2018.....	71
Jedwali Na. 7:	Mapato kutokana na Uwindaji wa Kitalii kuanzia Mwaka 2015 hadi 2017 ....	71
Jedwali Na. 8:	Mwenendo wa Upandaji miti katika Mashamba ya Miti nchini kwa Mwaka 2013/2014 hadi Machi, 2018.....	72
Jedwali Na. 9:	Mauzo ya Asali na Nta Ndani na Nje ya Nchi kwa Mwaka 2010/2011 – 2016/2017 .....	73
Jedwali Na. 10:	Mwenendo wa Biashara ya Utalii Nchini 2013-2017.....	73
Jedwali Na. 11:	Idadi ya Wageni Waliotembelea Vituo vya Mambo ya Kale na Mapato yaliyopatikana kwa Kipindi cha 2013/2014 hadi Machi, 2018.....	74
Jedwali Na. 12:	Takwimu za Wageni Waliotembelea Makumbusho ya Taifa na Mapato kwa mwaka 2015/2016 hadi Machi, 2018.....	75
Jedwali Na. 13:	Mapato Yatokanayo na Vibali vya Utafiti wa Raslimali za Malikale na Utafutaji wa Tunu kwa Mwaka 2013/2014 hadi Machi, 2018.....	76
Jedwali Na. 14:	Idadi ya Wanafunzi Waliodahiliwa katika Vyuo vya Wizara katika Kipindi cha 2013/2014 hadi 2017/2018.....	76

## 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, Ninaomba kutoa hoja kwamba kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu lipitishie Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

2. **Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena. Aidha, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kwa upekee, ninamshukuru kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kunateua kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Vilevile, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa maelekezo anayoyatoa ambayo yanatoa dira ya uhifadhi, ukuaji wa uchumi na ustawi wa wananchi. Pia, ninawashukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kwa miongozo wanayonipatia katika kutekeleza majukumu yangu kikamilifu.

3. **Mheshimiwa Spika**, Ninapenda kukupongeza wewe binafsi, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb), na Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb) na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha Bunge kwa weledi mkubwa.

4. **Mheshimiwa Spika**, Ninachukua fursa hii pia kuwashukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Nape Moses Nnauye (Mb), Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Kemirembe Julius Lwota (Mb) na Wajumbe wote wa Kamati kwa kuendelea kutupatia ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Kamati ilipata fursa ya kukutana na Wizara na kutembelea baadhi ya maeneo ya maliasili, malikale na vivutio vya utalii. Kupitia fursa hizo,

Kamati imeendelea kujiridhisha na kushauri namna ya kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zake.

**5. Mheshimiwa Spika,** Ninawapongeza Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel (Mbunge wa Jimbo la Siha), Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro (Mbunge wa Songea Mjini), Mheshimiwa Maulid Mtulia (Mbunge wa Jimbo la Kinondoni), Mheshimiwa Justine Joseph Monko (Mbunge wa Singida Kaskazini), na Mheshimiwa Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa (Mbunge wa Longido), kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa kuwa Mawaziri na Naibu Mawaziri. Niruhusu pia kuwashukuru Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga (Mb), Naibu Waziri; Meja Jenerali Gaudence S. Milanzi, Katibu Mkuu; na Dkt. Aloyce K. Nzuki, Naibu Katibu Mkuu; kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu yangu. Vilevile, ninawashukuru Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Mashirika na Taasisi, watumishi na wadau kwa ushirikiano wanaotupatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

**6. Mheshimiwa Spika,** Ninawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Nzega Vijijini kwa kuendelea kuniunga mkono kwa dhati katika kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge na Waziri wa Maliasili na Utalii. Ninapenda kuwahimiza kufanya kazi kwa bidii ili kuleta maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Aidha, nitakuwa mchoyo wa shukran bila kumshukuru kwa dhati mke wangu Dkt Bayoum Kigwangalla na familia yangu kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

**7. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Bunge lako Tukufu liliondokewa na Mheshimiwa Leonidas T. Gama, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Songea Mjini. Aidha, kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kushambuliwa na wanyamapori; ajali za vyombo vya usafiri kama vile mabasi na ndege; maradhi na majanga, kuna Waheshimiwa Wabunge, wananchi, watumishi na watalii waliojeruhiwa, waliopata ulemavu wa kudumu na waliofariki. Hivyo, ninaungana na wenzangu kuwapa pole wote waliopatwa na majanga na kufiwa na ndugu, jamaa na wapendwa wao. Ninamuomba Mwenyezi Mungu awajalie afya

njema waliojeruhiwa na azipumzishe roho za Marehemu Wapendwa Wetu mahala pema peponi – Amina.

**8. Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi, ninaomba kuwasilisha hotuba yangu ambayo imegawanyika katika sehemu kuu tano: **Kwanza,** Dira, dhima na majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii; **Pili,** umuhimu wa maliasili, malikale na utalii; **Tatu,** maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii; **Nne,** utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018; na **Tano,** Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

## **2.0 DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA**

**9. Mheshimiwa Spika,** Dira ya Wizara ya Maliasili na Utalii ni *“Maliasili na Malikale Zilizohifadhiwa kwa Manufaa ya Watanzania Wakati Ikiongoza Kuchangia Ukuaji wa Uchumi”*. Aidha, Dhima ya Wizara ni *“Uhifadhi Endelevu wa Maliasili na Malikale na Kuendeleza Utalii kwa Manufaa ya Taifa”*.

**10. Mheshimiwa Spika,** Ili kufanikisha Dhima yake, Wizara imeendelea kutekeleza malengo yake ya kulinda maliasili, malikale na kuendeleza utalii; kujenga uwezo wa kutekeleza majukumu yake; kuhakikisha wananchi na wadau wanashirikishwa; kukusanya maduhuli; na kuhakikisha Sekta ya Utalii inachangia katika ukuaji wa uchumi na kuongeza Pato la Taifa. Malengo ya Wizara yanatekelezwa kupitia Sera, Sheria na Kanuni, Mikakati, Programu na Miongozo.

**11. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaundwa na idara za maliasili na malikale (Wanyamapori, Misitu na Nyuki, na Mambo ya Kale) na utalii; Mashirika ya Hifadhi za Taifa (Tanzania National Parks - TANAPA) na Makumbusho ya Taifa (National Museum of Tanzania - NMT); Mamlaka za Hifadhi ya Ngorongoro (Ngorongoro Conservation Area Authority - NCAA) na Usimamizi wa Wanyamapori (Tanzania Wildlife Management Authority - TAWA); Wakala za Chuo cha Taifa cha Utalii (National College of Tourism - NCT), Mbegu za Miti (Tanzania Tree Seed Services Agency - TTSA) na Huduma za Misitu (TFS); Taasisi za utafiti wa Wanyamapori (Tanzania Wildlife Research Institute - TAWIRI) na Misitu (TAFORI); Bodi ya Utalii

(Tanzania Tourist Board - TTB); vyo vya usimamizi wa maliasili na utalii; na mifuko ya uhifadhi wa wanyamapori (Tanzania Wildlife Protection Fund - TWPF), misitu (Tanzania Forest Fund - TaFF), Mambo ya Kale (National Antiquities Fund - NAF), na Tozo ya Maendeleo ya Utalii (Tourism Development Levy - TDL).

### **3.0 UMUHIMU WA MALIASILI, MALIKALE NA UTALII**

#### **3.1. Maeneo ya Maliasili na Malikale**

**12. Mheshimiwa Spika,** Tanzania imejaliwa kuwa na maeneo ya maliasili na malikale yenye umuhimu mkubwa kimazingira, kiuchumi, na kijamii. Maeneo hayo ni pamoja na: hifadhi za wanyamapori, misitu na nyuki; na malikale. Maeneo ya Hifadhi za wanyamapori yamegawanyika katika makundi manne ambayo ni: Hifadhi za Taifa (16); Mapori ya Akiba (28); Mapori Tengefu (42); na Hifadhi ya Ngorongoro. Aidha, yapo maeneo 38 ya Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori (*Wildlife Management Areas – WMAs*) ambayo yanasimamiwa na Jumuiya za Jamii Zilizoidhinishwa (*Authorized Associations*). Vilevile, kuna maeneo ya wazi yenye wanyamapori ambayo ni shoroba, na mtawanyiko.

**13. Mheshimiwa Spika,** Maeneo ya misitu yanakadiriwa kuwa na hektari milioni 48.1. Kati ya hizo, asilimia 93 ni misitu ya mataji wazi (woodlands) na asilimia saba ni misitu iliyofunga. Aidha, misitu hiyo inakadiriwa kuwa na uwezo wa kukidhi uzalishaji wa takribani tani 138,000 za asali na tani 9,200 za nta kwa mwaka. Ufugaji nyuki unafanyika katika mikoa yote nchini, hata hivyo, uzalishaji mkubwa wa mazao ya nyuki unatoka kwenye mikoa 13 ambayo ni Tabora, Kigoma, Dodoma, Singida, Katavi, Shinyanga, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Iringa, Mbeya na Ruvuma.

**14. Mheshimiwa Spika,** Malikale ni raslimali za urithi wa utamaduni zinazoshikika na zisizoshikika; zinazohamishika na zisizohamishika; na zilizo nchi kavu na majini. Aidha, malikale ni vielelezo vya kisayansi, kiutamaduni na kiteknolojia vinavyohusu chimbuko na maendeleo ya binadamu. Zaidi ya maeneo 500 ya malikale yenye sifa tofauti yamegunduliwa hadi sasa. Kati ya maeneo hayo, 133 yametangazwa kuwa Urithi wa Taifa na maeneo matatu ni Urithi wa Dunia

(Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara; Michoro ya Miambani Kolo-Kondoa; na Bonde la Ngorongoro).

**15. Mheshimiwa Spika,** Ustawi wa sekta ya utalii unategemea pamoja na mambo mengine, uwepo wa maliasili, malikale na mazingira yaliyohifadhiwa vizuri. Sekta ya utalii ni muhimu katika kuchangia Pato la Taifa, kutoa ajira, kuingiza fedha za kigeni, kuchochea ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi kama vile kilimo, elimu, maji, mifugo, nishati (kuni, mkaa, na umeme), mawasiliano, miundombinu, michezo na burudani, usafirishaji na uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa watalii.

### **3.2. Mchango wa Maliasili, Malikale na Utalii katika Mazingira na Uchumi**

**16. Mheshimiwa Spika,** Huduma za maliasili kwa mazingira zimeainishwa katika Tathmini ya Mazingira ya Millenia (*Millennium Ecosystem Assesment*). Huduma hizo zinajumuisha: **Moja**, utoaji wa huduma kwa mazingira (*Provisioning Services*) kupitia uzalishaji wa vyakula (nyama na matunda), nishati, ujenzi, baio-kemikali na upatikanaji wa dawa; **Mbili**, huduma za kusaidia mazingira (*Supporting services*) ambazo ni pamoja na kuzalisha udongo wenye rutuba na kuzungusha virutubisho vyenye kuwezesha ustawi wa msingi na uhai wa mfumo mzima wa dunia; **Tatu**, huduma za udhibiti wa mazingira (*Regulating Services*), hususan udhibiti wa hali ya hewa na kupunguza hewa ukaa; na **Nne**, huduma za kitamaduni (*Cultural Services*) ambapo utamaduni wa wananchi unahusianishwa na mazingira ya maeneo yanayohifadhiwa.

**17. Mheshimiwa Spika,** Uhai wa binadamu na viumbe wengine unategemea uwepo wa uoto wa asili. Maliasili na mazingira husaidia kuthibiti mmomonyoko wa ardhi, kusafisha maji, kuzuia milipuko ya magonjwa na majanga ya asili. Uchumi wa Tanzania unategemea pamoja na mambo mengine, ardhi, maji, misitu na hewa safi. Wananchi wanayo fursa ya kuchangia katika ukuaji wa uchumi, kupunguza umasikini na kuenzi historia na utamaduni wa Mtanzania kupitia matumizi endelevu ya maliasili na malikale; biashara ya utalii; na ufugaji nyuki. Aidha, maliasili na malikale zinatoa mchango mkubwa katika elimu na maarifa, burudani na thamani za kiuchumi.

**18. Mheshimiwa Spika,** Kutokana na mwenendo wa uharibifu wa maliasili na mazingira, akiba ya mbegu za nyasi ardhini kwenye maeneo mengi hapa nchini imepungua. Hali hiyo imeathiri mzunguko wa virutubisho vya mimea na kusababisha madhara kwenye mazingira. Kwa kutambua umuhimu wa maliasili, malikale, mazingira na utalii, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ameendelea kusesitiza umuhimu wa kulinda maliasili za nchi, kuongeza jitihada za kupambana na ujangili na upotevu wa mazao ya misitu, kutatua migogoro ya mipaka kati ya vijiji na hifadhi, kutumia utalii kujenga uchumi na kuboresha mifumo ya ukusanyaji mapato.

**19. Mheshimiwa Spika,** Huduma za usafiri wa anga na utangazaji ni muhimu katika kuendeleza utalii. Kutokana na umuhimu huo, Mheshimiwa Rais ameendelea kutoa maelekezo ya kuimarisha Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) na kuanzisha Chaneli maalum kwa ajili ya kutangaza utalii katika Kituo cha Televisheni ya Taifa (TBC1). Maelekezo hayo yanaenda sanjari na azma ya Serikali ya kukuza utalii, kuongeza wigo kijiografia, na kutangaza fursa za uwekezaji. Aidha, jitihada nyingine za Serikali zinazoelekezwa katika ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja, viwanja vya ndege, na TEHAMA zimeendelea kujenga mazingira wezeshi katika kukuza utalii wa kimataifa na wa ndani. Ninayapongeza mashirika ya ndege na televisheni nyingine na wadau kwa kutambua umuhimu na kushiriki katika kusafirisha wageni, kuwekeza na kutangaza vivutio vya utalii.

**20. Mheshimiwa Spika,** Katika jitihada za kuendeleza uhifadhi wa maliasili na mazingira na faida zake, Mheshimiwa, Makamu wa Rais, ameendelea kusesitiza kuhusu umuhimu wa kuwahamasisha, kuwaelimisha na kuwashirikisha wananchi. Aidha, amesisitiza kuhusu ushirikiano kati ya mamlaka mbalimbali za Serikali na wananchi, Taasisi na Asasi za Kiraia na wadau katika kuheshimu na kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni. Vilevile, Makamu wa Rais amezitaka Mamlaka katika ngazi mbalimbali kutayarisha mipango ya matumizi bora ya ardhi, mikakati ya uhifadhi wa vyanzo vya maji, na kudhibiti uvunaji holela na ufugaji usio endelevu.

**21. Mheshimiwa Spika,** Katika kutatua migogoro kati ya wananchi na hifadhi na kukuza utalii, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maelekezo kuhusu umuhimu wa

kutambua chimbuko la migogoro ya ardhi na kuitatua kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu. Aidha, ameendelea kusesitiza kuhusu kuimarisha sekta ya utalii kwa kuwavutia wawekezaji zaidi; kuimarisha miundombinu ya maeneo ya utalii; na kuhamasisha utalii wa ndani ukiwemo utalii wa mambo ya kale na kihistoria katika miji ya kihistoria ya Bagamoyo, Kilwa na Mikindani.

**22. Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia maagizo ya Viongozi Wakuu wa Nchi, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwemo Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa na Wilaya ili kuhakikisha maliasili na malikale zinahifadhiwa na kulindwa kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa. Ninapenda kutoa rai kwa wananchi tuendeleo kujenga mtazamo chanya na kushirikiana katika kuhifadhi maliasili, malikale na kuendeleza utalii kwa ajili ya uhai na maendeleo ya Taifa letu na Dunia kwa ujumla.

#### **4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**

**23. Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilipitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, Kamati ilichambua mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kutoa maoni na ushauri uliolenga kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

**24. Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo 14 kama ifuatavyo: Kupitia Sera, Sheria na Kanuni ili zikidhi matakwa ya uhifadhi na maendeleo; kuimarisha usimamizi wa maliasili na malikale; kuimarisha usimamizi wa miradi ya maendeleo; kuongeza kasi na ushirikishaji katika utatuzi wa migogoro; kujenga uwezo wa Mashirika na Taasisi; kusimamia ukusanyaji mapato; kutambua na kuboresha miundombinu na vivutio vya utalii na kuvitangaza; kuimarisha utoaji wa mafunzo; kuzuia uvunaji haramu na usio endelevu wa maliasili; kuzuia uharibifu wa maeneo ya malikale; kuimarisha ushirikishwaji wa wadau; kuwekeza katika mipango ya matumizi bora ya ardhi; na kusimamia kikamilifu uwindaji wa kitalii na

Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (*Wildlife Management Areas - WMAs*).

**25. Mheshimiwa Spika,** Ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri wa Kamati umezingatiwa katika Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 ninayowasilisha leo hapa Bungeni.

## **5.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

**26. Mheshimiwa Spika,** Ninaomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Sehemu hii inafafanua vipengele vya ukusanyaji maduhuli, matumizi ya kawaida na maendeleo katika kutekeleza kazi zilizopangwa.

### **5.1 Ukusanyaji Maduhuli**

**27. Mheshimiwa Spika,** Wizara na Taasisi zilizo chini yake iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya Shilingi Bilioni 63.6. Hadi kufikia Machi 2018, jumla ya Shilingi Bilioni 32.0 sawa na asilimia 50 ya makadirio zilikusanywa. Kiasi kilichokusanywa ni ongezeko la asilimia 128 ikilinganishwa na Shilingi Bilioni 14 zilizokuwa zimekusanywa katika kipindi kama hicho cha mwaka 2016/2017. Baadhi ya sababu za kuongezeka kwa makusanyo hayo ni kuimarika kwa mifumo ya ukusanyaji maduhuli ya Serikali, kutangaza vivutio vya utalii, na kuboresha miundombinu ikiwemo barabara na hoteli.

**28. Mheshimiwa Spika,** Mashirika ya TANAPA, NCAA, TAWA na TFS yanayotekeleza majukumu ya uhifadhi, yanakusanya na kutumia fedha kwa ajili ya kujiendesha, na yanachangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Mashirika hayo yaliwekewa lengo la kukusanya Shilingi Bilioni 456.1 katika mwaka 2017/2018. Hadi Machi 2018, Mashirika hayo yamefanikiwa kukusanya Shilingi Bilioni 430 sawa na asilimia 94 ya makadirio.

## **5.2 Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

**29. Mheshimiwa Spika,** Wizara iliidhinishiwa kutumia Shilingi Bilioni 149.0 kwa matumizi ya kawaida na maendeleo. Fedha zilizotengwa kwa matumizi ya kawaida ni Shilingi Bilioni 97.2 na Shilingi Bilioni 51.8 zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi 2018, jumla ya Shilingi Bilioni 72.9 sawa na asilimia 49 ya bajeti iliyoidhinishwa zilipokelewa. Kati ya fedha zilizopokelewa, fedha za matumizi ya kawaida ni Shilingi Bilioni 45.0 na fedha za maendeleo ni Shilingi Bilioni 27.9.

## **5.3 Mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni**

**30. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kukamilisha mapitio ya Sera za Taifa za Misitu (1998) na Utalii (1999). Hadi Machi, 2018 Wizara imekamilisha rasimu za Sera hizo. Aidha, maandalizi ya kupitia Sheria ya Misitu yanaendelea sambamba na kutunga Sheria mpya ya Malikale ili ziendana na mabadiliko ya kiuchumi, kiteknolojia na kijamii yanayotokea ndani na nje ya nchi. Vilevile, Wizara inatunga Sheria mpya za Uhifadhi wa Wanyamapori na zinazosimamia TANAPA, NCAA na TAWA ili ziendane na Sheria mama za uhifadhi.

**31. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeandaa Kanuni mpya za Usimamizi wa Shoroba na Maeneo ya Wazi yenye wanyamapori na kukamilisha mapitio ya Kanuni za Uwindaji wa Kitalii. Aidha, Kanuni za Biashara ya Nyara na Wanyamapori Hai, WMA, na Mkataba wa CITES zinapitiwa. Mapitio hayo yanalenga kuhakikisha kuwa biashara hizo zinafanyika kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu; na kudhibiti biashara ya wanyamapori na mimea iliyo hatarini kutoweka.

**32. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeboresha Kanuni ya Ada na Tozo za Utalii kwa kushusha kiwango cha malipo kutoka Shilingi za kitanzania sawa na Dola za Marekani 2,000 kwa gari tano hadi kufika Shilingi sawa na Dola za Marekani 500 kwa gari moja hadi tatu. Kutokana na mabadiliko hayo, idadi ya wakala wa usafirishaji watalii imeongezeka kutoka 606 (2017) hadi 706 (Aprili, 2018). Aidha, Wizara imekamilisha rasimu ya Kanuni za kusimamia watoa huduma katika sekta ya utalii na ukarimu ili kuboresha huduma zitolewazo kwa watalii.

## **5.4 Majukumu ya Wizara na Taasisi zake**

### **5.4.1. Sekta Ndogo ya Wanyamapori**

**33. Mheshimiwa Spika,** Jukumu kuu la Sekta ndogo ya Wanyamapori ni kuhifadhi wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa kisheria. Jukumu hilo linatekelezwa kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Wanyamapori ya mwaka 2007, Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Sura 283, Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282 na Sheria ya Hifadhi ya Ngorongoro Sura 284.

**34. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa jukumu la Sekta umejikita katika kuhifadhi, kujenga uwezo wa Taasisi, na watumishi, kushirikisha wadau, kukusanya mapato na kuboresha mifumo ya usimamizi. Kazi hizo zimeteklezwa na Idara ya Wanyamapori, TAWA, TANAPA, NCAA, TAWIRI, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - Mweka, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi na Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga. Aidha, wananchi, sekta binafsi, Washirika wa Maendeleo na wadau wengine wameshirikishwa kikamilifu.

#### **5.4.1.1 Utekelezaji wa Masuala Mahsusi ya Sekta Ndogo ya Wanyamapori**

##### **i. Mkakati wa Usimamizi wa Pori Tengefu Loliondo**

**35. Mheshimiwa Spika,** Itakumbukwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu aliagiza Wizara ya Maliasili na Utalii kuunda chombo maalum kitakachosimamia Eneo la Pori Tengefu Loliondo kwa malengo mapana ya uhifadhi, maendeleo ya wananchi, wawekezaji wa shughuli za utalii na maendeleo ya sekta nyingine muhimu za kiuchumi bila migongano. Kwa kuzingatia agizo hilo, Wizara imeandaa rasimu ya Mkakati wa Usimamizi wa Pori Tengefu Loliondo unaoonesha muundo wa chombo cha kusimamia eneo husika na majukumu yake. Rasimu hiyo itawasilishwa kwa Mawaziri wanaohusika ili waidhinisha na kuwasilisha kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

## ii. Usimamizi wa Biashara ya Wanyamapori Hai

**36. Mheshimiwa Spika,** Serikali ilisitisha biashara ya wanyamapori hai Mei, 2016. Kwa kuzingatia ahadi ya Wizara katika hotuba ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara imeendelea kuchukua hatua kadhaa ikiwemo kuandaa mpango madhubuti wa kusimamia na kudhibiti uendeshaji wa biashara ya wanyamapori hai. Mpango huo unahusisha uwekaji wa mfumo wa ki-elektroniki wa utoaji wa vibali, ukusanyaji wa maduhuli na ufuatiliaji wa biashara ya wanyamapori hai. Aidha, Wizara inarekebisha Kanuni husika kwa lengo la kuweka wazi utoaji huduma na kuanzisha utaratibu wa kusimamia kwa karibu kazi ya ukamataji wa wanyamapori hai.

**37. Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hatua zinazoendelea kuchukuliwa kuimarisha mifumo ya usimamizi, Serikali imeridhia kuwarudishia wafanyabiashara walioathirika kutokana na usitishwaji huo fedha ambazo walizitumia kufanya malipo kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali. Kiasi cha Shilingi milioni 173.3 zinatarajiwa kulipwa baada ya uhakiki kukamilika. Hatua inayofuata ni kufanya utafiti utakaonesha hali halisi ya wanyamapori na kushauri kuhusu biashara ya wanyamapori hai.

## iii. Uwindaji wa Kitalii

**38. Mheshimiwa Spika,** Biashara ya uwindaji wa Kitalii inasimamiwa na TAWA ambayo inagawa vitalu na kutoa leseni kwa kampuni ambazo zimesajiliwa. Vitalu vya uwindaji vipo 159 ambavyo kati yake vitalu 78 vimekodishwa kwa kampuni na vitalu 81 vipo wazi. Katika msimu wa uwindaji (Julai hadi Desemba 2017), wawindaji wa kitalii 473 na wasindikizaji 291 walishiriki katika uwindaji. Aidha, kumekuwepo na changamoto ya vitalu kurejeshwa kwa sababu mbalimbali. Kufuatia hali hiyo, Wizara imeanza kufanya yafuatayo: i) kuimarisha ulinzi katika Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu ili kurejesha hadhi yake; ii) kuongeza muda wa kumiliki vitalu; iii) kuruhusu shughuli za utalii wa picha kufanyika baada ya msimu wa uwindaji kwisha; iv) kupitia upya viwango vya tozo na ada za leseni mbalimbali; na v) kubadili sheria ya uwiano wa kampuni za wazawa na wageni.

**39. Mheshimiwa Spika,** Kwa kutambua umuhimu wa tasnia ya uwindaji wa kitalii katika kukuza uchumi wa nchi, Wizara kupitia TAWA imeendelea kurekebisha muundo wa uwekezaji na utaratibu wa kugawa vitalu vya uwindaji. Hatua hiyo inahitaji mabadiliko ya Sheria ya Wanyamapori ambayo imeanza kufanyiwa kazi.

**iv. Kuzuia na Kupambana na Ujangili**

**40. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kusimamia na kuratibu operesheni za kuzuia na kupambana na ujangili kupitia Kikosikazi cha Kuzuia Ujangili (*National Anti-poaching Task Force*). Kikosikazi hicho kinatekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na TANAPA, NCAA, TAWA na TFS. Kazi hiyo inatekelezwa kwa kuzingatia taarifa za kiintelijensia na TEHAMA ikiwemo ndege zisizokuwa na rubani (drones) na mbwa wa kunusa. Kutokana na operesheni hizo, watuhumiwa 505 wamekamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria. Aidha silaha 143 za aina mbalimbali na meno ya tembo yenye uzito wa kilo 371 yamekamatwa.

**v. Udhibiti wa Mifugo kwenye Maeneo ya Hifadhi**

**41. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia Sheria ili kudhibiti uingizaji wa mifugo ndani ya maeneo ya hifadhi za wanyamapori na misitu kinyume cha sheria. Kutokana na hatua hiyo, uoto wa asili umeanza kurejea kwenye maeneo mbalimbali na ustawi wa wanyamapori umeendelea kuimarika. Mafanikio hayo yameanza kuonekana katika Mapori ya Akiba ya Burigi, Biharamulo na Kimisi. Aidha, Wizara imewasilisha mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya uhifadhi wa wanyamapori ili kuoanisha na kurahisisha utoaji wa adhabu kwa makosa yatokanayo na kuingiza na kuchunga mifugo ndani ya hifadhi.

**vi. Ulinzi wa Wananchi na Mali zao Dhidi ya Wanyamapori Wakali na Waharibifu**

**42. Mheshimiwa Spika,** Serikali inatambua umuhimu wa kulinda maisha ya wananchi na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu. Aidha, zoezi la kuhakiki athari zitokanazo na uharibifu wa wanyamapori huchukua muda mrefu. Vilevile, uhaba wa fedha za kuhakiki na kulipa waathirika umekuwa ni changamoto.

Ili kukabiliana na changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu, Wizara kupitia TANAPA, NCAA, na TAWA imeendesha doria katika maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kuwalinda wananchi na mali zao. Pia, Wizara imeanza kutekeleza mpango wa kutumia teknolojia na mbinu mbalimbali. Mathalan, ndege zisizo na rubani (*Unmanned Aerial Vehicle*) na kuendelea kuhamasisha matumizi ya pilipili na ufugaji nyuki kuzuia wanyamapori hususan tembo kuingia maeneo ya wananchi. Aidha, Wizara inaandaa mabadiliko ya Sheria na taratibu zinazolenga kuongeza ufanisi katika uhakiki na upatikanaji wa fedha za kifuta jasho na kifuta machozi kwa wakati.

**43. Mheshimiwa Spika,** Sanjari na hatua hizo, Wizara imeanza maandalizi ya ujenzi wa vituo vya askari, (ranger posts) kwenye maeneo yenye matukio ya mara kwa mara ya wanyamapori wakali na waharibifu kama vile Wilaya ya Bunda, Tarime, Itilima, na Serengeti. Aidha, Wizara imeendelea kuchangia katika kusogeza huduma za kijamii karibu na wananchi (maji, afya, na elimu). Mathalani, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi imewezeshwa kuchimba visima tisa vya maji kwa ajili ya wananchi wanaoishi kando kando ya Mto Ruvuma. Hatua hizo zinachukuliwa ili kuwanusuru wananchi kutokana na madhara ya wanyamapori wakali ikiwemo mamba wakati wakitafuta maji katika mto huo. Majukumu hayo yanatekelezwa na Wizara kupitia Mashirika ya TANAPA, NCAA, TAWA, na kwa ushirikiano na Mamlaka nyingine za Serikali.

#### **vii. Usimamizi wa Pori Tengefu Kilombero**

**44. Mheshimiwa Spika,** Bonde la Kilombero ambalo linajumuisha ardhievu inayotambuliwa kimataifa (Ramsar site) na Eneo la Pori Tengefu ni eneo la lindimaji linalochangia maji katika Mto Rufiji. Bonde hilo lina utajiri wa kuwepo na aina zaidi ya 400 za ndege na mnyamapori aina ya Sheshe (Puku) ambaye ni adimu. Aidha, Bonde hilo ni chanzo muhimu cha maji kwa shughuli za kibinadamu na maendeleo ikiwemo Mradi wa uzalishaji wa Umeme wa Maji Rufiji (Rufiji Hydropower Project). Pamoja na umuhimu huo, Bonde hilo linakabiliwa na changamoto za uvamizi kwa ajili ya shughuli za kibinadamu. Kutokana na hali hiyo, Wizara imeunda kamati maalum ili kuishauri Serikali hatua za kutatua changamoto hizo.

### **viii. Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA)**

**45. Mheshimiwa Spika,** Sera ya Taifa ya Wanyamapori (2007) inaelekeza ushirikishaji wananchi katika uhifadhi wa wanyamapori na kuwanufaisha. Katika kutekeleza azma hiyo, Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) uhifadhi wa wanyamapori nje ya maeneo ya hifadhi kwa kuwasimasha wananchi kuanzisha maeneo ya Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori (WMAs). Jumla ya WMAs 22 zimesajiliwa na kupewa haki ya matumizi (user rights) na 16 zipo katika hatua mbalimbali ya uanzishaji. Madhumuni ya kuanzisha WMA ni: i) Kuimarisha uhifadhi wa wanyamapori kwenye maeneo ya shoroba na mtawanyiko; ii) Kuhakikisha WMA zinakuwa na nguvu ya kisheria; na iii) Kuwanufaisha wananchi.

**46. Mheshimiwa Spika,** Dhana ya WMA imeendelea kupata mafanikio licha ya changamoto zinazojitokeza ambazo ni pamoja na ujangili, uvamizi kwa matumizi mengine ya ardhi na usimamizi dhaifu. Mathalani, kati ya WMA 22 zilizosajiliwa, zinazofanya vizuri ni Mbarang'andu (Namtumbo), Burunge (Babati), Enduiment (Longido), Ikona (Serengeti), Ipole (Sikonge), MAGINGO (Liwale), Makao (Meatu), Ngarambe/Tapika (Rufiji), Uyumbu (Urambo), na RANDILEN (Monduli). Aidha, Jamii zimeendelea kuhamasika katika kushiriki kwenye uanzishaji na usimamizi wa WMA. Vilevile, wananchi wameweza kuhifadhi na kunufaika na WMA zilizoimarishwa kimfumo na kujengewa uwezo wa usimamizi. Kupitia uhifadhi wa wanyamapori, wananchi wameweza kupata huduma za kijamii kama vile afya, elimu, maji, ajira za muda mfupi na mrefu pamoja na soko la bidhaa na huduma mbalimbali zinazozalishwa katika maeneo hayo.

**47. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuzijengea uwezo Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori kwa kutoa mafunzo ya namna ya kuziendesha WMA. Mafunzo hayo yametolewa kwenye WMA za Mpimbwe (Mlele), Makame, Waga (Mufindi, Iringa na Mbarali), JUHIWANGUMWA (Rufiji), Ziwa Natron (Longido), ILUMA (Ulanga na Kilombero) na Kidoma (Mvomero na Kilosa).

#### 5.4.1.2 Idara ya Wanyamapori

**48. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Wanyamapori inatekeleza jukumu la urekebu, kudurusu na kusimamia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya uhifadhi wa wanyamapori.

**49. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuandaa Mpango wa Usimamizi wa Spishi zilizo hatarini kutoweka (*Species Action Plan*). Spishi hizo ni simba, duma, chui na mbwa mwitu. Aidha, Wizara inaboresha Mpango wa Usimamizi wa tembo, faru na sokwe. Mipango hiyo inalenga kuwa na mikakati ya pamoja badala ya kuwa na mpango wa kila Spishi. Sanjari na hatua hiyo, Wizara imeendelea kutumia mbinu za kisasa za kukabiliana na uvunaji na usafirishaji haramu wa wanyamapori waliopo hatarini kutoweka. Pia, Wizara imeendelea kuimarisha vituo vya ukaguzi katika bandari na viwanja vya ndege. Hatua hiyo imeviwezesha vituo hivyo kufanya kazi kwa saa 24.

#### 5.4.1.3 Shirika la Hifadhi za Taifa

**50. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Hifadhi za Taifa linatekeleza jukumu la uhifadhi, kusimamia na kuendeleza utalii kwenye Hifadhi za Taifa 16 zenye eneo la kilometa za mraba 57,365.8. Katika kuimarisha ulinzi na kudhibiti ujangili katika Hifadhi, Shirika limeendesha jumla ya siku doria 103,914 ambapo majangili 2,607 na silaha 11 aina ya SMG zimekamatwa. Aidha, ujenzi wa vituo vya kutolea taarifa kwa watalii katika Hifadhi za Taifa Serengeti na Udzungwa umekamilika. Vilevile, ujenzi wa vituo vitatu vya kupumzika wageni, nyumba za kulala wabeba mizigo na vyoo 11 katika Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro, na ujenzi wa nyumba ya malazi nafuu katika Hifadhi ya Taifa Kitulo unaendelea.

**51. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeongeza juhudi za kutangaza utalii katika hifadhi za taifa kupitia vyombo vya habari vya ndani na nje. Shirika limeweka mabango ya kuhamasisha utalii katika barabara ya Arusha - KIA (4); na viwanja vya ndege JNIA (17), KIA (64) na Arusha (2).

**52. Mheshimiwa Spika,** Shirika limejenga nyumba 30 za watumishi katika Hifadhi za Taifa Arusha (1), Gombe (3), Kilimanjaro (3), Kitulo (2), Manyara (2), Mahale (1), Ruaha (1), Rubondo (2), Saadani (9), Serengeti (5) na Udzungwa (1). Aidha, Shirika limetengeneza barabara zenye urefu wa kilometa 682.5. Vilevile, daraja la Rukoma linalopakana na barabara ya Kigoma kuelekea Hifadhi ya Taifa Mahale limejengwa.

**53. Mheshimiwa Spika,** Shirika limetekeleza Programu ya Ujirani Mwema kwa kuchangia miradi katika vijiji 33 vinavyozunguka Hifadhi za Taifa. Miradi hiyo ni vyumba vya madarasa (30), nyumba za walimu (6), visima vya maji (5), zahanati (1) na kituo cha Polisi (1). Vilevile, majengo ya utawala (2), bwalo la chakula (1), matumizi ya majiko banifu katika vijiji (5), na kuanzisha vitalu vya miche ya miti (16). Aidha, Shirika limewezesha vikundi 20 vya kiuchumi na kuvipatia mizinga ya ufugaji nyuki 660 Vijiji 12 na kusaidia vijiji 2 kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Wilaya zilizofaidika na Programu hiyo ni Korogwe, Mwanga, Meru, Karatu, Makete, Same, Mlele, Lushoto, Bagamoyo, Kigoma Vijijini, Geita, na Moshi Vijijini.

#### **5.4.1.4 Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro**

**54. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro inatekeleza jukumu la kuhifadhi, kuendeleza jamii za wafugaji wenyeji na mifugo, na kuendeleza utalii. Katika kuimarisha ulinzi na kudhibiti ujangili, Mamlaka imeendesha jumla ya siku za doria 66,900 ambapo majangili 34 wamekamatwa. Aidha, Mamlaka imeendelea kuhakikisha maeneo ya vivutio vya utalii yanafikika kwa kuendelea kukarabati barabara za ndani na nje ya bonde la Kreta. Vilevile, Mamlaka imekamilisha maandalizi ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara kutoka lango la Loduare (NCAA) yenye urefu wa Kilometa 88 kuelekea lango la Naabi (Hifadhi ya Taifa Serengeti). Kufuatia maendeleo hayo, Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) limeridhia kujengwa kwa barabara hiyo kwa kiwango cha lami kwenye Hifadhi ya Ngorongoro ambalo ni Urithi wa Dunia.

**55. Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa jengo la kitega uchumi la Mamlaka katika Jiji la Arusha umekamilika. Lengo ni kufanya Jengo hilo kuwa kituo kimoja cha kutoa huduma za utalii (*Tourism One Stop Centre*) ili kurahisisha upatikanaji wa utoaji huduma za utalii. Kufuatia hatua hiyo, Mamlaka imeanza kutangaza na kupata wapangaji wa Jengo hilo.

**56. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imekamilisha miradi ya maji katika maeneo ya Mbitini, Ndepesi na Olduvai. Aidha, Mamlaka imetekeleza miradi mingine kwa ajili ya wenyeji ikiwemo ujenzi wa lambo moja (Ndepesi) na uchimbaji wa visima viwili vya maji (Oldonyogol olduvai na Ngoile - Kata ya Olbalbal). Vilevile, kituo cha Askari kinajengwa katika eneo la Nasera Rock ambapo ujenzi huo umekamilika kwa asilimia 95.

**57. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) imefanya Sensa ya watu, makazi na mifugo katika Tarafa ya Ngorongoro ili kubaini idadi ya wakazi halali na mifugo ndani ya Hifadhi. Sensa hii itasaidia kutambua uwezo wa eneo kuhimili idadi ya watu na mifugo ili kukidhi malengo ya uhifadhi. Aidha, Asilimia 60 ya wenyeji wanaoishi ndani ya Hifadhi wamepewa vitambulisho vya Taifa. Ili kudhiti uingizaji holela wa mifugo ndani ya Hifadhi, ng'ombe 201,203 kati ya 238,845 wamekwa alama ya utambulisho. Mamlaka imeendelea kutoa huduma za chanjo za kuzuia ugonjwa wa kimeta kwa ng'ombe, mbuzi na kondoo wapatao 300,000. Pia, huduma ya chanjo imetolewa kwa ndama 1,600 (Ndigana kali - ECF) na mbwa 2,140 (kuzuia kichaa - Rabies).

**58. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imelipatia Baraza la Wafugaji shilingi 782,087,500 kwa ajili ya kuwasomesha wanafunzi 1,235 kuanzia ngazi ya elimu ya msingi hadi chuo kikuu. Aidha, Mamlaka imetoa huduma ya afya kwa wenyeji 8,916 kupitia zahanati ya Mamlaka na Hospitali ya Enduleni ambapo jumla ya shilingi milioni 450 zimetolewa kwa hospitali ya Enduleni.

#### **5.4.1.5 Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania**

**59. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania inatekeleza jukumu la kusimamia uhifadhi wa wanyamapori kwenye Mapori ya Akiba (28), Mapori Tengefu (42), na maeneo ya wazi yenye wanyamapori yanayojumuisha shoroba na mtawanyiko. Aidha, Mamlaka inashirikiana na jamii katika kusimamia maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (38) na maeneo manne ya Ardhievu (Ramsar Sites). Usimamizi wa maeneo haya unafanywa kwa kutumia Mpango Mkakati (2018/19 - 2022/23) ambao unatoa mwelekeo wa kufikia malengo yanayohusu kuimarisha uhifadhi, kuendeleza utalii na kuboresha uwezo wa taasisi.

**60. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha uwezo kitaasisi, mafunzo ya aina mbalimbali yametolewa kwa watumishi 200. Mafunzo haya ni pamoja na mbinu za kiintelijensia, uchunguzi, ufuatiliaji na tathmini; ununuzi na ugavi; uongozi; na usimamizi wa fedha. Aidha, Mamlaka imenunua magari 53, pikipiki 15 na boti nne, na imepokea magari 10 kutoka kwa wahisani kwa ajili ya kuwezesha utekeleza wa majukumu yake.

**61. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha ulinzi wa wanyamapori, hadi Machi, 2018 Mamlaka imeendesha siku doria 190,042 katika maeneo yanayosimamiwa na Mamlaka. Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama imefanya doria maalum katika maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Wami-Mbiki; Pori Tengefu Loliondo na Mapori ya Akiba Moyowosi-Kigosi na Uwanda. Katika doria hizo, watuhumiwa wa ujangili 4,208 wamekamatwa na kesi 2,465 zimefunguliwa. Vilevile, meno ya tembo yenye uzito wa kilo 895.16 yamekamatwa. Pia, bunduki za rashasha 279; risasi 2,278; mitego 7,170; magari sita; pikipiki 73; baiskeli 317; mifugo 30,892; magobore 2; na mitumbwi 112 imekamatwa.

**62. Mheshimiwa Spika,** Katika kuwalinda wanyamapori hususan tembo wanaohama kutoka Pori la Akiba Selous kuelekea Pori la Niassa Msumbiji, shoroba za Litumbandyosi na Gesimasowa zilizopo Mkoa wa Ruvuma yatapandishwa hadhi

na kuwa Mapori ya Akiba. Hatua hiyo imeungwa mkono na Serikali za vijiji, Wilaya na Mkoa wa Ruvuma. Aidha, WMA ya Wami-Mbiki inapandishwa hadhi kuwa Pori la Akiba ili kulinda wanyamapori wanaohama kati ya Hifadhi za Taifa za Mikumi na Saadani; na Pori la Akiba Selous. Hatua hizo zinabadilisha hadhi ya maeneo ya Hifadhi bila kuchukua maeneo mapya ya wananchi.

**63. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imelipa jumla ya **Shilingi 837,071,100** kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali. Malipo hayo ni kwa ajili ya fidia kwa wananchi 308 wa kitongoji cha Machimbo kijiji cha Mabadaga Wilaya ya Mbarali waliokuwa wanaishi ndani ya Pori la Akiba Mpanga-Kipengele wakati wa uanzishwaji wake. Ni matarajio ya Wizara kwamba, Halmashauri ya Mbarali kwa kushirikiana na Menejimenti ya Pori la Akiba Mpanga Kipengele na wananchi wanaohusika itafanikisha ulipaji wa fidia hizo.

**64. Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza utalii, Mamlaka imeendelea kuboresha miundombinu hususan barabara za kuvinjari na viwanja vya ndege; kuandaa miongozo; na kutenga maeneo ya uwekezaji na kushiriki katika kutangaza utalii. Kutokana na juhudi hizo, jumla ya watalii 97,494 wametembelea Mapori ya Akiba Ikorongo/Grumeti na Selous; Mapori Tengefu Loliondo na Ziwa Natron; maeneo ya wazi ya Losirwa na Olasiti; na maeneo ya Hifadhi za Jamii (WMA) za Enduiment, Burunge, Randilen na Ikona.

#### **5.4.1.6 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania**

**65. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania inatekeleza jukumu la kusimamia, kufanya na kuratibu utafiti wa wanyamapori na ufugaji nyuki. Aidha, Taasisi hutoa ushauri kuhusu uhifadhi endelevu wa wanyamapori kwa kutumia matokeo ya utafiti wa kisayansi.

**66. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imeratibu miradi 126 yenye watafiti 332, ambapo miradi 119 inatekelezwa na Watanzania. Aidha, Taasisi imeendelea kutekeleza miradi 34 ikiwemo ya utafiti wa mbwa mwitu, na utafiti wa magonjwa ya kimeta, homa ya vipindi na kifua kikuu. Vilevile, Taasisi imeendelea na utafiti wa jinsi

mfumo wa ikolojia Serengeti unavyofanya kazi na manufaa yake kwa jamii, utafiti wa mahusiano ya nyuki na mimea, na sensa za wanyamapori.

**67. Mheshimiwa Spika,** Mbwa mwitu wapo katika tishio la kutoweka hapa nchini. Utafiti wa Mbwa Mwitu katika mfumo ikolojia - Serengeti umeendelea kwa kufuatilia makundi 24 yenye jumla ya mbwa mwitu 277. Makundi hayo yanatumia maeneo ya Hifadhi za Serengeti, Ngorongoro, Mapori ya Akiba Maswa na Ikorongo/Grumeti, Mapori Tengefu Loliondo na Ziwa Natron, na maeneo ya Selela na Engaruka. Lengo la utafiti huu ni kurejesha uwiano wa kiikolojia unaotokana na mchango wa wanyama hao ambao miaka ya 1990 walitoweka katika Mfumo wa Ikolojia – Serengeti. Aidha, mbwa hao ni miongoni mwa vivutio muhimu vya utalii. Utafiti umebaini kuwa mbwa mwitu 19 walikufa katika Hifadhi ya Serengeti kwa ugonjwa wa kifafa cha kanivora (*Canine Distemper Virus*). Vilevile, Wizara imeendelea kuelimisha jamii za wafugaji kuhusu jinsi ya kujilinda dhidi ya mbwa mwitu.

**68. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imeendelea na utafiti kuhusu uwezo wa mfumo ikolojia - Serengeti kuhimili ongezeko la tembo katika kipindi cha miaka 50 ijayo. Matokeo ya utafiti huo yatatolewa katika mwaka wa fedha 2018/2019 na yatasaidia katika kuandaa Mpango Kabambe wa Kuhifadhi Tembo katika mfumo ikolojia - Serengeti. Aidha, utafiti kuhusu mfumo ikolojia hiyo umebaini kuna idadi kubwa ya mifugo ambayo haiendani na malisho katika eneo la magharibi mwa mfumo ikolojia - Serengeti. Kutokana na matokeo hayo inashauriwa kuwa mifugo ipunguzwe katika eneo hilo.

**69. Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kuwepo kwa taarifa za vifo vya mifugo katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Taasisi imefanya uchunguzi na kubaini kuwa vifo hivyo vimesababishwa na ukame, magonjwa na wingi wa mifugo kuliko uwezo wa eneo. Mifugo iliyokufa ni 236,437 (ng'ombe 77,889; kondoo 78,490; mbuzi 72,881; na punda 7,177) sawa na wastani wa asilimia 28.3 ya mifugo yote. Aidha, uchunguzi umebaini kuwa ugonjwa wa kimeta kwa mifugo umesababisha madhara makubwa kwa jamii ya wafugaji waliokula nyama ya mifugo hiyo. Vilevile, watu 240 waliugua kimeta na kati yao 18 walifariki. Uchunguzi huu unadhihirisha kuwa kuna

madhara makubwa ya mwingiliano kati ya binadamu, wanyamapori na mifugo. Kutokana na hali hiyo, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imechukua hatua ya kutoa chanjo kwa mifugo yote na kuwaelimisha wafugaji.

**70. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imeendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Maabara ya Utafiti wa Ufugaji Nyuki ambao unakaribia kukamilika. Aidha, Taasisi imeendelea na utafiti wa mimea na nyuki wanaouma na wasiouma katika Wilaya 120. Matokeo ya awali ya utafiti huu yametumika kuchora ramani ya kiikolojia inayoonesha kanda muhimu za ufugaji nyuki nchini. Vilevile, matokeo yameainisha aina mbalimbali za asali katika kanda na maeneo mbalimbali. Pia, Kituo kimetoa huduma za ushauri kwa wafugaji nyuki 378. Aidha, Kituo kimetoa mafunzo kuhusu njia sahihi za ufugaji wa nyuki kwa vijiji vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa Tarangire na Hifadhi ya Ngorongoro.

#### **5.4.1.7 Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori – Mweka**

**71. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - Mweka kinatekeleza jukumu la kutoa mafunzo, ushauri wa kitaalam na kufanya utafiti kuhusu uhifadhi wa wanyamapori na uendeshaji utalii. Chuo kimedahili wanafunzi 551. Aidha, Chuo kimeendesha kozi fupi kwa wadau wa ndani na nje ya nchi na kutayarisha mtaala ambao umewasilishwa kwenye Kamisheni ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) kwa ajili ya kuidhinishwa (Accreditation). Vilevile, Chuo kimekamilisha ujenzi wa nyumba mbili katika eneo la Kwakuchinja kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo, kukarabati nyumba tano za watumishi, jengo la mafunzo na mabweni ya wanafunzi. Pia, kimenunua magari mawili makubwa kwa ajili ya usafiri wakati wa mafunzo kwa vitendo.

#### **5.4.1.8 Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori – Pasiansi**

**72. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori - Pasiansi inatekeleza jukumu la kutoa mafunzo ya uhifadhi wa wanyamapori katika ngazi ya Astashahada. Taasisi imedahili wanachuo 441 kati ya hao 394 ni katika ngazi ya Astashahada ya Awali ya Uhifadhi wa Wanyamapori na 47 ni ngazi ya Astashahada ya Uhifadhi wa Wanyamapori. Aidha, Taasisi imetoa mafunzo ya muda mfupi kuhusu

intelijensia, upelelezi, uhifadhi wa wanyamapori na usimamizi wa sheria kwa washiriki 107 kutoka Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (62) na Jumuiya tano za Kuhifadhi Wanyamapori (45).

#### **5.4.1.9 Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu – Sekamaganga**

**73. Mheshimiwa Spika,** Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu –Sekamaganga kinatekeleza jukumu la kuzijengea uwezo jamii zinazoishi jirani na maeneo yenye wanyamapori ili ziweze kushiriki katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili. Kituo kimetoa mafunzo kwa Askari Wanyamapori wa Vijiji (47), na Viongozi wa Kamati za Maliasili za vijiji (8). Aidha, Kituo kimetoa mafunzo kwa wananchi (42) kutoka wilaya za Serengeti, Tunduru na Meatu yanayohusu mbinu za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu. Vilevile, Kituo kimetayarisha Mtaala wa kozi ya Astashahada ya awali ya waongoza watalii na kuuwasilisha NACTE kwa ajili ya kuthibitishwa.

#### **5.4.1.10 Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania**

**74. Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania unatekeleza jukumu la kuwezesha uhifadhi wa wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Hadi Machi 2018, Mfuko umewezesha doria na upelelezi unaofanywa na Kikosikazi cha Taifa cha Kudhibiti na Kupambana na Ujangili na biashara haramu ya wanyamapori. Aidha, Mfuko umewezesha kulipa fedha za kifuta jasho na kifuta machozi, kufanya uhakiki wa matukio yaliyosababishwa na wanyamapori waharibifu, mafunzo, utafiti, na kulipa ada za mikataba ya kimataifa.

#### **5.4.2 Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki**

**75. Mheshimiwa Spika,** Jukumu kuu la Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki ni kuhifadhi na kusimamia misitu iliyopo ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa na kuendeleza ufugaji nyuki. Jukumu hilo linatekelezwa kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya

Misitu, 1998; Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki, 1998; Sheria ya Misitu Sura 323; na Sheria ya Ufugaji Nyuki Sura 224.

**76. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa jukumu la Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki umejikita katika kulinda na kuendeleza misitu na ufugaji nyuki, kujenga uwezo wa watumishi na Taasisi, kushirikisha wadau, kukusanya mapato, na kuboresha mifumo ya usimamizi. Utekelezaji wa kazi hizo umefanyika kupitia Idara ya Misitu na Nyuki; Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS); Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania (TTSA); Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI); Chuo cha Misitu, Olmotonyi (FTI); Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora (BTI); Chuo cha Viwanda vya Misitu, Moshi (FITI); na Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF). Aidha, wananchi, sekta binafsi, Washirika wa Maendeleo na wadau wengine wameshirikishwa kikamilifu.

#### **5.4.2.1 Utekelezaji wa Masuala Mahsusi ya Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki**

##### **i. Kupandisha hadhi Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania**

**77. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeanza maandalizi ya kupandisha hadhi Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania kuwa Mamlaka ya Misitu Tanzania. Uamuzi huu unalenga kuimarisha usimamizi wa misitu ya asili inayomilikiwa na Serikali Kuu, Halmashauri za Wilaya, na Serikali za Vijiji. Aidha, utekelezaji wa azma hii unazingatia haja ya kujenga mfumo madhubuti wa usimamizi wa misitu na ufugaji nyuki; kupitia miundo ya mamlaka mbalimbali za usimamizi wa misitu na nyuki; matumizi bora ya ardhi vijijini; na kuwa na chombo kimoja kitakachosimamia misitu ya hifadhi. Vilevile, tathmini inafanyika ili kuainisha misitu inayopaswa kupandishwa hadhi kuwa chini ya usimamizi wa Serikali Kuu.

##### **ii. Kuongeza Mashamba ya Miti**

**78. Mheshimiwa Spika,** Uanzishaji wa mashamba mapya ya miti ni kati ya miongoni mwa mikakati ya kuongeza upatikanaji wa malighafi ya viwanda vya misitu, mapato na ajira. Katika kutekeleza azma hiyo, Wakala umeanzisha Mashamba mapya manne yenye ukubwa wa hektari 76,967. Mashamba hayo ni: Chato-Biharamulo, hektari 50,000 (Chato); Mpepo, hektari 2,017 (Mbinga); Iyondomsimwa,

hektari 12,000 (Ileje); na Pagale, hektari 12,950 (Mvomelo). Katika mashamba hayo mapya jumla ya hektari 1,335 zimepandwa miti. Hatua hii imeongeza idadi ya mashamba ya Serikali kutoka 18 hadi 23. Mashamba haya yametoa ajira 90,000 za moja kwa moja na 50,000 zisizo za moja kwa moja kwa wananchi.

### **iii. Kuboresha Miundombinu ya Utalii Ikolojia**

**79. Mheshimiwa Spika,** Katika kuboresha utalii ikolojia kwenye maeneo ya misitu, ujenzi wa ngazi na eneo la kupumzika katika maporomoko ya mto Kalambo unaendelea. Aidha, njia za kutembea kwa miguu katika hifadhi za mazingira asilia ya Mlima Hanang, Mlima Uluguru, Mkingu na Rondo zimejengwa. Vilevile, ujenzi wa majengo ya ofisi sita za wahifadhi na vituo (*Ranger outposts*) 15 unaendelea katika hifadhi za Chome, Mlima Rungwe, Magamba, Mkingu, Minziro na Uzungwa Scarp, ambapo ujenzi umefikia zaidi ya asilimia 80. Pia, Hifadhi 12 zimepatiwa vifaa vya kisasa vya mawasiliano na usafiri. Wakala umeandaa mipango ya usimamizi wa bioanuai na uendelezaji utalii. Pia, Misitu ya Hifadhi za Kalambo, Ituli na Uvinza inapandishwa hadhi kuwa Misitu ya Hifadhi ya Mazingira Asilia.

### **iv. Nishati Inayotokana na Kuni na Mkaa**

**80. Mheshimiwa Spika,** Zaidi ya asilimia 85 ya nishati yote nchini inatokana na kuni na mkaa ambapo takribani asilimia 90 ya wananchi wote hutegemea nishati hiyo. Hali hiyo inatokana na utegemezi mkubwa wa misitu ya asili kama chanzo kikuu na rahisi cha nishati na mapato kupitia biashara ya utengenezaji na uuzaji mkaa, kuni, mbao, na nguzo.

**81. Mheshimiwa Spika,** Katika kupunguza utegemezi huo, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuchukua hatua zifuatazo: kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala kama gesi na *briquettes*; kufundisha namna ya utengenezaji wa majiko banifu ya kutumia kuni na mkaa; kubaini maeneo ya misitu yenye miti inayofaa kwa utengenezaji wa mkaa; kufundisha mbinu bora za utengenezaji wa mkaa; na kuandaa maeneo maalum ya uuzaji wa mkaa (kwa mfano, vituo vya Maguha na Berega kwenye barabara kuu ya Dodoma – Morogoro);

kuwatambua watengenezaji na wauzaji wa mkaa, na kuhamasisha wananchi na makundi mbalimbali ya watu kupanda miti kwa ajili ya kuzalisha kuni na mkaa.

**82. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhimiza taasisi zenye matumizi makubwa ya nishati ya kuni na mkaa kwa mfano, Hospitali, Shule na Vyuho, na Majeshi (Polisi, Magereza, JKT, JWTZ) kutumia nishati mbadala na teknolojia zinazobana matumizi ya nishati.

**v. Kiwanda cha Kuzalisha Karatasi cha Mufindi (Mufindi Paper Mills)**

**83. Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha kuzalisha karatasi cha Mufindi (Mufindi Paper Mills - MPM) kilibinafsishwa mwaka 2004 kwa Kampuni ya RAI Group ya Kenya. Kabla ya ubinafsishaji, Kiwanda hakikufanya kazi kwa miaka 14. Hali hiyo ilisababisha miti iliyokuzwa kwa ajili ya karatasi kufikia umri wa miaka 25 ambayo inafaa zaidi kwa ajili ya uzalishaji wa magogo ya mbao. Aidha, wakati ubinafsishaji wa kiwanda unafanyika mkataba wake uliainisha kuwa Serikali itahakikisha kuwa kiwanda kinapata kiasi cha malighafi ya miti kisichozidi meta za ujazo 500,000 kila mwaka. Mkataba wa mauziano ya kiwanda haukuainisha viwango vya tozo na ada za malighafi ya kiwanda.

**84. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza mkataba huu, kumekuwepo na changamoto ya kukosekana kwa miti inayofaa kuzalisha miti ya tetefya (pulpwood), inayofaa kwa karatasi. Hivyo, kulazimika kutumia miti inayofaa kuzalisha magogo ya mbao ambayo tozo na ada zake ni kubwa kuliko zile za miti ya tetefya. Aidha, Kampuni haikuweka mkakati wa kuzalisha malighafi yake ya kutosha kutokana na eneo la kuotesha miti kwa ajili ya matumizi ya kiwanda kuvamiwa na vijiji jirani. Kutokana na hali hiyo, Kampuni haipo tayari kununua malighafi kwa tozo na ada za miti inayofaa kuzalisha magogo ya mbao. Katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizo, Wizara yangu imeunda kikosikazi kitakacho chambua na kushauri kuhusu masuala yafuatayo: mtiririko wa mahitaji na matumizi halisi ya kiwanda, viwango vya tozo na ada za malighafi ya kiwanda, uwezo wa shamba la Sao Hill kuhudumia kiwanda na wateja wengine, na kupitia mkataba kati ya Serikali na kiwanda.

#### **5.4.2.2 Idara ya Misitu na Nyuki**

**85. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Misitu na Nyuki inatekeleza jukumu la kutayarisha na kusimamia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya usimamizi wa misitu na ufugaji nyuki.

**86. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa umma, kwa ushirikiano na Halmashauri za Wilaya kuhusu upandaji miti na ufugaji nyuki kupitia sherehe za kitaifa za kupanda miti na kutundika mizinga. Sherehe ya kitaifa ya kutundika mizinga ilifanyika tarehe 3 Oktoba 2017 wilaya ya Itilima mkoa wa Simiyu. Aidha, maadhimisho ya siku ya kupanda miti kitaifa yamefanyika wilaya ya Kishapu, Shinyanga kuanzia tarehe 3 hadi 5 Aprili, 2018.

#### **5.4.2.3 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania**

**87. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania unatekeleza jukumu la kusimamia, kuhifadhi misitu na kuendeleza ufugaji nyuki. Wakala unasimamia misitu ya hifadhi ya asili, misitu iliyo katika maeneo yasiyohifadhiwa (Forests on General land), mashamba ya miti na hifadhi za nyuki za Serikali Kuu. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wakala unaongozwa na Sheria ya Wakala Sura 245, Tangazo la Kuanzisha Wakala Na. 269/2010, Sheria ya Misitu Sura 323 na Sheria ya Ufugaji Nyuki Sura 224.

**88. Mheshimiwa Spika,** Wakala umekamilisha mipango ya usimamizi wa misitu ya hifadhi ya Ruvu Kaskazini (Kibaha) na Kimboza (Morogoro). Aidha, mipango ya usimamizi wa misitu ya Nawenge, Mkulazi na Mamiwa Kusini (Kilosa); Mtapwa (Lindi); Ruhifwe (Tanganyika); na Liwilikitesa (Mbinga Vijijini) ipo katika hatua za ukamilishaji. Vilevile, kazi ya tathmini na kukusanya takwimu za misitu 25 imefanyika kwa ajili ya kutayarisha mipango ya usimamizi.

**89. Mheshimiwa Spika,** Katika kuzuia uharibifu wa uoto wa asili, vyanzo vya maji na bioanuwai, Wakala umeendelea kuwaondoa wavamizi kwenye hifadhi. Aidha, Wakala umeendelea kudhibiti uvunaji holela na biashara haramu ya mazao ya misitu kwa kuendesha doria. Hadi Machi 2018, wavamizi wameondolewa katika misitu 33

ambapo wahalifu 3,834 na mifugo 33,544 ilikamatwa. Jumla ya kesi 43 kati ya 117 zilizofunguliwa zimetolewa hukumu. Katika operesheni hizo, baadhi ya mali zilizokamatwa ni magunia 1,383 ya mkaa, vipande 300 vya magogo, mbao 1,963 na misumeno ya minyororo 10. Aidha, matanuru 257 ya mkaa na kambi 25 za watengeneza mkaa ziliharibiwa. Kutokana na hatua hizo, uoto wa asili umeanza kurejea kwenye maeneo hayo.

**90. Mheshimiwa Spika,** Hadi Machi 2018, jumla ya siku doria 13,527 zimeendeshwa kwa kufanya kazi za ufuatiliaji wa kiintelijensia, ukaguzi na udhibiti wa biashara ya mazao ya misitu kwenye maeneo ya uvunaji na masoko. Kupitia doria hizo, mazao na bidhaa za misitu yaliyovunwa na kumilikiwa kinyume cha Sheria ya Misitu yalikamatwa. Mazao na bidhaa hizo ni magunia 58,057 ya mkaa, magogo 6,350, vipande vya mbao 57,775, milango 829 na, nguzo 13,239.

**91. Mheshimiwa Spika,** Wakala umevuna asali yenye uzito wa kilo 6,519 na Nta yenye uzito wa kilo 281 kutoka katika manzuki (*apiaries*) 143 zenye mizinga 9,448. Aidha, elimu imetolewa kwa wadau 656 kuhusu njia bora za kuongeza mnyororo wa thamani kupitia uvunaji, uchakataji na ufungashaji (*packaging*). Vilevile, asali ya Tanzania imefanyiwa uchambuzi wa kimaabara na kuthibitika kuwa inakidhi viwango vya soko la nje ya nchi. Kutokana na matokeo hayo, Tanzania imeendelea kuruhusiwa kuuza asali kwenye soko la nchi za Jumuiya ya Ulaya.

**92. Mheshimiwa Spika,** Katika kuboresha miundombinu na mazingira ya kazi, Wakala umejenga ofisi mbili na kukarabati nyumba 40 za kuishi watumishi katika vituo mbalimbali. Aidha, Wakala umesafisha kilomita 1,329 za barabara na kutengeneza barabara mpya kilomita 99 kwenye mashamba ya miti. Vilevile, magari 14, boti mbili na mitambo miwili ya kutengeneza barabara imenunuliwa.

**93. Mheshimiwa Spika,** Wakala umetoa elimu kwa umma kupitia uchapishaji na usambazaji wa nakala 30,000 za machapisho mbalimbali, na vipindi 41 vya redio na 54 vya televisheni. Elimu na uhamasishaji uliotolewa unahusu madhara ya uharibifu wa misitu kwa mazingira; kuzuia moto wa msituni; uzalishaji, uchakataji na

ufungashaji wa mazao ya nyuki; na utaratibu wa biashara ya mazao ya misitu na nyuki.

#### **5.4.2.4 Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania**

**94. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania unatekeleza jukumu la kuzalisha na kusambaza mbegu bora za miti na vipandikizi kwa ajili ya upandaji miti hapa nchini na kuuza ndani na nje ya nchi. Wakala unatekeleza jukumu hilo kupitia vituo vyake vya Morogoro, Iringa, Lushoto na Shinyanga.

**95. Mheshimiwa Spika,** Wakala umekusanya mbegu za miti zenye uzito wa tani 14 ambapo tani 10 zimeuzwa. Aidha, miche 2,800,000 ilizalishwa na kuuzwa kwa wadau mbalimbali. Katika kuhakikisha upatikanaji endelevu wa mbegu za miti ya mbao, Wakala kwa kushirikiana na TFS na TAFORI umeanzisha vyanzo vipya vya mbegu za miti aina ya Mkongo na Mkangazi. Vilevile, vyanzo vipya nane vya mbegu za Misindano na Mikaratusi vimeanzishwa katika mashamba ya miti ya Rongai (Kilimanjaro), Shume (Tanga) na Ipogolo (Iringa); na Wilaya za Songea, Madaba, Mbinga, Nyasa na Ludewa. Pia, Wakala umeendelea kuboresha vyanzo vya mbegu za miti aina ya Misindano, Mikaratusi, Mkongo na Mkangazi.

#### **5.4.2.5 Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania**

**96. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania inatekeleza jukumu la kufanya na kuratibu utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu matumizi ya teknolojia bora na uendelezaji wa misitu. Taasisi imeendelea kufanya utafiti kwenye Nyanja tatu: i) Kubaini umri sahihi wa kuvuna miti ya Misindano na ubora wa mbao kutoka katika mashamba ya miti ya Rubare (Bukoba vijijini), Rubya (Ukerewe) na Buhindi (Sengerema); na ii) Kubaini chanzo halisi cha kukauka kwa miti aina ya Misindano na Grevilea katika Kanda ya Kaskazini; na iii) Kufanya tathmini ya wadudu waharibifu wa miti aina ya Mikaratusi ya kloni Wilaya za Muheza, Korogwe na Handeni.

**97. Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa: i) Umri wa uvunaji wa miti aina ya misindano kwa ajili ya matumizi ya mbaao ni kati ya miaka 18 hadi 20 badala ya miaka 25, na miaka 11 kwa ajili ya kuzalisha karatasi; ii) Miti ya Misindano na *Grevilea* iliyopandwa kwenye Shamba la Miti Kilimanjaro Magharibi lililopo Wilaya ya Siha, inakauka kutokana na ugonjwa wa kuoza mizizi (*Root rot disease*) unaosababishwa na fangasi jamii ya *Armillaria*; na iii) Utunzwaji sahihi wa mashamba ya miti ya Mikaratusi na matumizi ya viatilifu vinavyoweza kuzuia na kuuwa wadudu. Matokeo ya utafiti yanatumiwa na wadau katika uendelezaji na matumizi endelevu ya mazao ya misitu.

**98. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imekusanya na kusambaza taarifa kuhusu janga la moto wa misitu kwa kutumia takwimu za *satellite*. Taarifa inaonyesha kuwa janga la moto kwa misitu bado ni kubwa na limeathiri eneo la misitu lenye kilometa za mraba 101,955 katika mkoa ya Katavi, Tabora, Kigoma na Mbeya. Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuelimisha umma kuhusu kuchukua tahadhari na kuzuia moto wa misitu.

**99. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imetoa elimu kuhusu upandaji na uhifadhi wa miti kwa ajili ya dawa kwa wananchi wa Wilaya za Chalinze, Handeni na Manispaa ya Dodoma kwa mfano mti wa Mnyenze (*Terminalia sericea*) ambao wananchi wamehamasika na kukubali kutenga maeneo kwa ajili ya kuutunza. Aidha, Taasisi imeanzisha utafiti wa mashamba ya mbegu bora za miti ya Misindano na Mkaratusi mwekundu katika Wilaya ya Lushoto, mkoa wa Tanga.

#### **5.4.2.6 Vyuho vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki**

**100. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Misitu Olmotonyi (Arusha), Chuo cha Viwanda vya Misitu (Moshi), na Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (Tabora) vinatekeleza jukumu la kutoa mafunzo ya uhifadhi, usimamizi na matumizi endelevu ya misitu na ufugaji nyuki katika ngazi ya Astashahada na Stashahada. Aidha, Chuo cha Misitu Olmotonyi kimetoa mafunzo ya muda mrefu kwa wanafunzi 672, kati yao 405 ni wa Astashahada na 267 ni wa Stashahada. Vilevile, Chuo cha Viwanda vya Misitu kimetoa mafunzo kwa wanafunzi 133, kati yao 113 ni wa Astashahada na 20

ni wa Stashahada. Vilevile, Chuo cha Ufugaji Nyuki kimetoa mafunzo kwa wanafunzi 201 katika ngazi za Astashahada (171) na Stashahada (30).

#### **5.4.2.7 Mfuko wa Misitu Tanzania**

**101. Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Misitu Tanzania umetoa ruzuku kwa miradi 204 kwenye nyanja zifuatazo: upandaji wa miti (65), ufugaji nyuki (92), upandaji miti na ufugaji nyuki (17), ushirikishwaji jamii katika usimamizi wa misitu (10), nishati mbadala na utumiaji wa majiko banifu (6), utafiti (10) na viwanda vya mazao ya nyuki (4). Miradi hiyo inatekelezwa kwenye Wilaya 81, na vijiji 399 katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara. Aidha, Mfuko umewezesha utoaji wa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa uhifadhi, uendelezaji na usimamizi endelevu wa misitu. Elimu hiyo imetolewa kwa kusambaza nakala 2,000 za Jarida la **Misitu ni Mali**; kuandaa na kurusha vipindi 24 kupitia Redio ya Taifa (TBC) na vipindi vinne kupitia Televisheni ya Taifa (TBC1).

**102. Mheshimiwa Spika**, Mfuko umechangia katika kujenga uwezo katika kusimamia hima-sheria, utafiti na mafunzo kwa kuzipatia baadhi ya Taasisi vitendea kazi kama magari (10) na vifaa vya maabara ya mbegu za miti. Aidha, Mfuko umewezesha ujenzi wa jengo la maktaba katika Chuo cha Viwanda vya Misitu, Moshi – FITI na ujenzi wa jengo la utawala katika Chuo cha Misitu Olmotonyi. Vilevile, Mfuko umewezesha ukarabati wa miundombinu ya kitalu cha miti kwa ajili ya mafunzo ya vitendo katika Chuo cha Misitu Olmotonyi.

#### **5.4.3 Sekta Ndogo ya Utalii**

**103. Mheshimiwa Spika**, Jukumu kuu la Sekta Ndogo ya Utalii ni kuendeleza utalii nchini, na kuhakikisha inachangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi na Pato la Taifa. Jukumu hilo linatekelezwa kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Utalii, 1999 na Sheria ya Utalii, Sura 29.

**104. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa jukumu la Sekta Ndogo ya Utalii umejikita katika kutambua, kuendeleza na kutangaza vivutio vya utalii; kujenga uwezo wa watumishi na Taasisi; kushirikisha wadau; kukusanya mapato na kuboresha mifumo ya usimamizi. Utekelezaji wa kazi hizo umefanyika kupitia Idara ya Utalii, Bodi ya Utalii Tanzania, na Chuo cha Taifa cha Utalii. Aidha, wananchi, sekta binafsi, Washirika wa Maendeleo na wadau wengine wameshirikishwa kikamilifu.

#### **5.4.3.1 Utekelezaji wa Masuala Mahsusi ya Sekta Ndogo ya Utalii**

##### **i. Kuandaa Utambulisho wa Tanzania Kimataifa (Destination Branding)**

**105. Mheshimiwa Spika,** Katika juhudi za kutangaza utalii, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kuandaa Utambulisho wa Tanzania Kimataifa (*Destination Branding*). Lengo la utambulisho huo ni kuitambulisha Tanzania kama kituo mahsusi cha utalii Duniani; kuvutia wageni wa kimataifa kuitembelea Tanzania; kuongeza wigo wa kutangaza vivutio; na kuvifanya vivutio vya utalii vya Tanzania vifahamike duniani. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara imeandaa Kauli Mbiu ya kuitangaza Tanzania katika masoko ya utalii ambayo ni “**Tanzania, Unforgettable**”. Hatua inayofuata ni kuandaa mionekano (*visuals*) ambayo itaelezea kwa undani na kwa urahisi vionjo vya vivutio mbalimbali vilivyopo nchini.

##### **ii. Uanzishaji wa “Studio” na Chaneli ya Utalii Tanzania**

**106. Mheshimiwa Spika,** Wizara inashirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo katika kuanzisha Chaneli maalum katika Televisheni ya Taifa (TBC1) kwa ajili ya kutangaza utalii. Aidha, Wizara inaendelea na maandalizi ya kuanzisha “Studio” ya kutangaza utalii kwa njia ya teknolojia ya habari na mawasiliano. Studio hiyo itawezesha kutambua, kufuatilia na kuwasiliana moja kwa moja na watu wanaofuatilia Tanzania na vivutio vyake kwa njia ya TEHAMA.

#### 5.4.3.2 Idara ya Utalii

**107. Mheshimiwa Spika,** Idara ya utalii inatekeleza jukumu la kusimamia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo kwa ajili ya maendeleo ya utalii.

**108. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea na kazi ya kupanga daraja za ubora wa huduma za malazi na chakula kwa viwango vya kati ya nyota moja hadi tano katika mikoa ya Arusha na Manyara. Baadhi ya faida ya kuweka huduma za malazi katika daraja za ubora ni: kuwezesha wageni kufahamu viwango vya ubora wanavyotarajia kupata, kupata urahisi wa kujitangaza kibiashara, na Serikali kufuatilia utoaji wa huduma kulingana na vigezo vya ubora.

**109.** Katika kutekeleza kazi hiyo, jumla ya huduma za malazi na chakula 230 zimefanyiwa tathmini. Kati ya hizo, 178 zimekidhi vigezo na kupangwa katika daraja za ubora kama ifuatavyo: nyota tano (10), nyota nne (19), nyota tatu (65), nyota mbili (81), na nyota moja (3). Aidha, Huduma 18 za malazi na chakula zimethibitishwa bila kupata daraja. Vilevile, huduma 34 za malazi na chakula hazikuthibitishwa kwa sababu hazikukidhi vigezo. Wizara imeendelea kutoa ushauri wa kitaalam ili huduma za malazi na chakula ambazo hazikufikia vigezo ziweze kuboreshwa kufikia kiwango kinachotakiwa.

**110. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kufanya ukaguzi wa wakala wa biashara za utalii ili kubaini wanaofanya biashara kinyume cha Sheria ya Utalii. Kazi hiyo imefanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Manyara, Morogoro, Dodoma, Singida, Tanga, Kilimanjaro, na Arusha. Aidha, kazi hiyo imetekelezwa kwenye malango ya kuingilia wageni ya Hifadhi za Taifa Kilimanjaro, Mikumi, Ngorongoro, na Pori la Akiba Selous. Katika ukaguzi huo, Wakala wa utalii 74 walibainika kuendesha biashara ya utalii bila leseni na kutakiwa kulipia ada ya leseni ambapo jumla ya Shilingi 189,252,000 zilikusanywa.

### 5.4.3.3 Bodi ya Utalii Tanzania

**111. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Utalii Tanzania inatekeleza jukumu la kutangaza utalii wa ndani na nje ya nchi kwa kuzingatia Sheria ya kuanzisha Bodi ya Utalii Sura 364.

**112. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhamasisha utalii wa ndani kwa kushirikiana na wadau kupitia Maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Saba saba) - Dar es Salaam; Serengeti Cultural Festival - Mara; Maonesho ya Kilimo (Nane nane) - Dodoma na Lindi; Wiki ya Utalii Duniani na Karibu Kusini - Iringa. Maonesho mengine ni kumbukumbu ya Vita vya Majimaji - Songea; Biashara ya kimataifa ya Afrika Mashariki - Mwanza; Hydrom Cultural Festival - Manyara; Tulia Traditional Festival - Mbeya; TASUBA Festival - Pwani; na Rock City Marathon - Mwanza. Aidha, Kampeni maalum ya kuhamasisha utalii wa ndani kwa kutumia kauli mbiu ***“Utalii wa ndani unaanza na mtanzania mwenyewe”*** ilifanyika kupitia redio na televisheni.

**113. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Bodi imeendelea kuandaa onesho la kimataifa la utalii lijulikanalo kama Swahili International Tourism Expo (SITE) ambalo kwa mwaka 2017/2018 lilifanyika kuanzia tarehe 13 hadi 15 Oktoba 2017, jijini Dar es Salaam. Onesho limekutanisha wafanyabiashara na mawakala wa utalii wa hapa nchini na wale wa kutoka Mauritius, India, Ethiopia, Romania, Urusi, Ujerumani, Ufaransa, Uingereza, Morocco, Kenya, Zambia, Malawi, Namibia, Nigeria, Zimbabwe, Uganda na Rwanda. Onesho hilo limeongeza wanunuzi wa safari kutoka 112 mwaka 2015 hadi 224 mwaka 2017. Aidha, idadi ya nchi zilizoshiriki zimeongezeka kutoka nchi 25 mwaka 2015 hadi 36 mwaka 2017 na kampuni za uoneshaji zimeongezeka kutoka 110 hadi kufikia 145.

**114. Mheshimiwa Spika,** Bodi kwa kushirikiana na Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania - TABOA imeanza utaratibu wa kutangaza vivutio vya utalii ndani ya mabasi ya abiria. Utangazaji huo ambao unafanyika kwa kutumia video umeanza mwezi Agosti, 2017 ambapo hadi Machi, 2018 jumla ya mabasi 352 yameanza kutoa huduma hiyo.

**115. Mheshimiwa Spika,** Utangazaji kwa watalii wa nje kwa kushirikiana na sekta binafsi umefanyika kupitia maonesho katika nchi za Uingereza (WTM); Uholanzi (Dutch Expo); India (OTM); Ujerumani (ITB); Urusi (MITT na LTF); China (COTTM); Afika Kusini (WTM); Dubai (ATM); na Uganda (JAMAFESTI). Aidha, Bodi imeratibu wanamichezo mashuhuri 10 wa filamu kutoka China kutengeza filamu ambayo inarushwa kwenye vituo vya Televisheni nchini China. Filamu hizo zimetengenezwa kwenye maeneo ya Dar-es-Salaam, Pemba, Pori la Akiba Selous, Kreta ya Ngorongoro na Hifadhi ya Serengeti. Vilevile, jumla ya waandishi wa habari 11 kutoka Israel wametembelea baadhi ya vivutio vya utalii ikiwemo Mji Mkongwe wa Zanzibar na Hifadhi ya Gombe.

**116. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha utalii wa michezo, Bodi kwa kushirikiana na kampuni ya Sport Pesa imeratibu ziara ya timu ya mpira wa miguu ya Everton ya Uingereza hapa nchini. Kufuatia ziara hiyo, wachezaji na waandishi wa habari wametembelea vivutio vya utalii vya Hifadhi ya Ngorongoro, Hifadhi ya Taifa ya Manyara na Makumbusho ya Taifa - Dar es Salaam na kuvitangaza katika mitandao ya timu ya Everton na ligi kuu ya mpira wa miguu ya Uingereza (English Premier League - EPL). Aidha, Bodi imeendelea kuhamasisha watu mashuhuri na maarufu kutembelea Tanzania. Kwa mfano, Rais wa Mauritius na Bwana Leon Osman mchezaji wa zamani wa Everton, walitembelea Tanzania katika mwaka huu wa fedha.

**117. Mheshimiwa Spika,** Bodi imeendelea kutoa ushauri wa kitaalam, hususan masoko, kwa vikundi vipya 10 vinavyoendesha utalii wa utamaduni (*Cultural Tourism Enterprises*) katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Tanga na Manyara na kufanya vikundi hivyo kufikia 76 hadi sasa. Vikundi vingine kama hivyo vimeanzishwa katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Dodoma, Ruvuma, Mara, Pwani, Lindi, Mwanza, Simiyu na Morogoro. Lengo la kuvisaidia vikundi hivyo ni kuviwezesha kushiriki na kunufaika na biashara ya utalii, kutangaza utamaduni wa Mtanzania na kujenga uzalendo.

**118. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia TTB, TANAPA, NCAA, na TAWA imeendelea kutangaza utalii kwa kuweka mabango makubwa katika maeneo ya kimkakati. Maeneo hayo ni: i) Majiji ya Dar es Salaam, Mwanza na Dodoma; ii) Viwanja vya ndege vya kimataifa vya JNIA, KIA na Songwe; iii) Maeneo ya hoteli kubwa za kitalii, mipaka, na viwanja vya michezo; iv) Makutano ya barabara na mzunguko (*roundabout*); na v) Eneo la Sirari, mpakani mwa Tanzania na Kenya.

#### **5.4.3.4 Chuo cha Taifa cha Utalii**

**119. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Taifa cha Utalii kilianzishwa kwa Sheria ya Wakala wa Serikali Sura 245. Jukumu la Chuo hicho ni kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri katika fani ya utalii na ukarimu.

**120. Mheshimiwa Spika,** Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 228 kati ya hao 209 ngazi ya Astashahada na 19 ngazi ya Stashahada. Aidha, wanafunzi 102 wamedahiliwa programu ya uanagenzi (*apprenticeship*) inayotolewa kwa kushirikiana na wadau wa Hoteli, Shirika la misaada la Norway (NORAD) na Shirika la Kazi la Umoja wa Mataifa (ILO). Vilevile, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 322 katika fani ya Utalii na Ukarimu. Wanafunzi 154 wamehitimu katika ngazi za Astashahada na Stashahada. Aidha, kwa kushirikiana na Chuo kikuu cha Vancouver (Kanada) kimeandaa mitaala ya uendeshaji matukio (*Event Management*) katika ngazi za astashahada na stashahada. Mitaala hii imewasilishwa Baraza la Elimu ya Ufundi Stadi (NACTE) kwa ajili ya kuidhinishwa.

#### **5.4.4 Sekta Ndogo ya Malikale**

**121. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika,** Jukumu kuu la Sekta Ndogo ya Mambo ya Kale ni kufanya utafiti, kutambua, kuhifadhi, kulinda, kuendeleza na kutangaza malikale. Sekta hiyo inasimamiwa na Sera ya Taifa ya Malikale 2008; Sheria ya Mambo ya Kale, Sura 333; na Sheria ya Makumbusho, Sura 281. Utekelezaji wa jukumu la Sekta ya Malikale umejikita katika kuhifadhi, kulinda na kuendeleza maeneo ya Malikale; na kujenga uwezo wa watumishi na Taasisi. Utekelezaji wa kazi hizo umefanyika kupitia Idara ya Mambo ya Kale na Shirika la

Makumbusho ya Taifa. Aidha, wananchi, sekta binafsi, Washirika wa Maendeleo na wadau wengine wameshirikishwa kikamilifu.

#### **5.4.4.1 Utekelezaji wa Masuala Mahsusi ya Sekta Ndogo ya Malikale**

##### **i. Kuendeleza Vituo vya Mambo ya Kale**

**122. Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza vituo vya mambo ya kale, Wizara imeandaa Mkakati wa Kuendeleza Maeneo ya Malikale. Maeneo ya kipaumbele ni: Laetoli, Engaruka, Mumba, Nasera na Engaresero; Mapango ya Amboni na Magofu ya Kunduchi. Maeneo mengine ni Nyumba ya Kumbukizi ya Mwalimu Nyerere, Caravan Serai na Kaole; Michoro ya Miambani ya Kondo; Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara, Isimila, Kalenga na Kimondo cha Mbozi; Tembe la Kwihara na *Old Afya Building*; na Kituo cha Livingstone Ujiji.

**123. Mheshimiwa Spika,** Mkakati huo utahusisha kuweka huduma muhimu kwa watalii, kuboresha miundombinu ya vituo hususan vituo vya kumbukumbu na taarifa, ofisi, mabanda ya kupumzika watalii na barabara ili viwe na muonekano unaovutia na kufikika kwa urahisi. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni kujenga vituo vya taarifa pale ambapo vitahitajika, kuandaa vionyeshwa, maonyesho na kutangaza vituo. Aidha, Mkakati huo utatekelezwa kwa ushirikiano na Mashirika ya TANAPA, NCAA, TAWA, TFS, TTB na NMT. Vilevile, wadau hususan sekta binafsi na wananchi watahirikishwa kikamilifu katika utekelezaji wake.

##### **ii. Tamasha la Urithi wa Taifa (Urithi Festival: Celebrating Our Heritage)**

**124. Mheshimiwa Spika,** Wizara imebuni maadhimisho ya Tamasha la Urithi wa Taifa (Urithi festival). Lengo la Tamasha hilo ni kunadi urithi na utamaduni wa Mtanzania ndani na nje ya nchi. Tamasha litajielekeza zaidi kwenye historia, utamaduni, malikale, lugha, chakula, mavazi, imani, mila na desturi. Wizara kwa kushirikiana na wadau imeanza maandalizi ya maadhimisho ya Tamasha hilo yatakayofanyika Septemba kila mwaka katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Katika kutekeleza azma hiyo, Kamati ya Kitaifa imeundwa ili kuratibu maandalizi ya

Tamasha hilo. Aidha, Tamasha litaongeza wigo wa mazao ya utalii kwa kunadi vivutio vya urithi wa taifa, kuongeza uelewa wa wageni kuhusu Tanzania na idadi ya siku ambazo watalii watakaa nchini.

**125. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara kupitia Kamati ya Kitaifa ya Maandalizi ya Tamasha imekamilisha kazi zifuatazo: kuandaa mwongozo wa kufanikisha tamasha kila mwaka; kuainisha shughuli zitakazotekelezwa; na kuwashirikisha wadau katika maandalizi na ufanikishaji wa Tamasha.

#### **5.4.4.2 Idara ya Mambo ya Kale**

**126. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mambo ya Kale inatekeleza jukumu la kutayarisha na kusimamia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya utafiti, uhifadhi na kuendeleza Malikale. Aidha, Idara inaratibu na kufanya utafiti, kutambua, kulinda, kuhifadhi, kuendeleza na kuelimisha wadau kuhusu umuhimu wa Malikale.

**127. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara – Mikindani, imetangaza Mji wa Kihistoria wa Mikindani kuwa Urithi wa Taifa kwa Tangazo la Serikali Na. 308 la tarehe 25 Agosti, 2017. Aidha, Wizara imehakiki mipaka ya Kituo cha Mapango ya Amboni na kuweka alama za kudumu (vigingi) katika eneo lenye ukubwa wa hekari 15.6. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Kituo cha Televisheni cha Channel Ten imeandaa na kurusha vipindi vinne vya televisheni kuhusu ushiriki wa wadau katika matumizi endelevu ya malikale katika Mkoa wa Tanga.

**128. Mheshimiwa Spika,** Wizara imekamilisha ujenzi wa kituo cha Kumbukumbu na Taarifa katika eneo la Kimondo cha Mbozi, mkoa wa Songwe. Aidha, Wizara imekamilisha michoro na makadirio ya gharama za ujenzi kwa ajili ya ukarabati wa Jengo la Kihistoria la Caravan Serai, Bagamoyo. Vilevile, Wizara imefungua Makumbusho mpya ya kisasa katika Bonde la Kihistoria la Olduvai katika eneo la Ngorongoro. Pia, Wizara imeboresha kituo kipya cha Engaruka ambacho kinahifadhi historia ya mfumo wa umwagiliaji wa kijadi wa karne ya 13 hadi 17.

**129. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeratibu utafiti wa malikale kwenye nyanja 54 za: akiolojia (3); palentolojia (4); akiolojia na palentolojia (4); na utafutaji wa tunu (43). Matokeo ya utafiti huo yatasaidia kuongeza idadi ya vivutio vya utalii wa malikale. Utafiti huo umetekelezwa kwenye mikoa ya Lindi, Iringa, Arusha, Mbeya, Manyara, Kilimanjaro, Tabora, Dar es Salaam na Njombe. Mikoa mengine ni Morogoro, Mwanza, Pwani, Katavi, Dodoma na Mtwara.

**130. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kukusanya taarifa za maeneo yaliyotumika wakati wa kupigania uhuru wa Nchi za Kusini mwa Afrika yaliyopo katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma. Maeneo hayo ni: shule za Sekondari Farm 17 na Matekwe; shule ya Msingi Majonanga, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Chilala na Jengo la kituo cha Polisi Rutamba yaliyopo mkoa wa Lindi. Aidha, katika mkoa wa Mtwara maeneo yaliyohusishwa ni Jengo la Wazazi – Hospitali ya Ligula; Mnara na makaburi ya Mashujaa Naliendele. Vilevile, katika mkoa wa Ruvuma shule ya Sekondari Masonya imehusishwa. Lengo la kukusanya taarifa hizo ni kuyatambua, kuyahifadhi na kutunza historia ya ukombozi wa Bara la Afrika na kuyaendeleza ili yawe vivutio vya utalii.

#### **5.4.4.3 Mfuko wa Mambo ya Kale**

**131. Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Mambo ya Kale umeendelea kutekeleza jukumu lake la kuwezesha uhifadhi, utafiti, uendelezaji na utangazaji wa malikale. Mfuko umewezesha ujenzi wa Kituo cha Kumbukumbu na Taarifa cha Kimondo - Mbozi na kuhakiki mipaka ya Kituo cha Amboni - Tanga.

#### **5.4.4.4 Shirika la Makumbusho ya Taifa**

**132. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Makumbusho ya Taifa linatekeleza jukumu la kutafiti, kuhifadhi, kukusanya, kuonesha na kuelimisha umma kuhusu urithi wa utamaduni na asili wa Taifa kwa mujibu wa Sheria ya Makumbusho ya Taifa Sura 281.

**133. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeboresha maonesho ya muda na ya kudumu katika makumbusho saba kwa kubadili vioneshwa, mipangilio ya maonesho na maelezo ya vioneshwa. Aidha, maonesho mawili ya kudumu kuhusu Chimbuko la Binadamu Afrika na Uzalendo katika Vita vya Majimaji yamefunguliwa. Vilevile, maonesho ya Karibu Tanzania Image, Harakati za Ukombozi wa Afrika, Vipepeo na Nondo Wachavushao, Mapambano Dhidi ya Rushwa, Kumbukizi ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na miaka 56 ya Uhuru wa Tanzania Bara yamefanyika.

**134. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeratibu maadhimisho ya kitaifa ya kumbukizi la vita vya Maji Maji na utalii wa utamaduni yanayofanyika Februari 27 kila mwaka Mkoa wa Ruvuma. Lengo la maadhimisho hayo ni kuwakumbuka na kuwaenzi mashujaa wa Vita vya Maji Maji, kuainisha vivutio vya utalii vilivyoko mikoa ya kusini na kuvitangaza.

**135. Mheshimiwa Spika,** Shirika limesajili mikusanyo 3,100 na taarifa zake kuhifadhiwa kwenye nakala laini. Kati ya mikusanyo hiyo, 696 ni mipya iliyotokana na ukusanyaji wa vipepeo (358), nondo (311) na mikusanyo mchanganyiko (27) kutokana na programu ya *Museum Art Explosion*. Aidha, masalia ya zamadamu yamehifadhiwa kwenye chumba imara (*strong room*) kwa kutumia vifaa maalum na kanzidata za masalia hayo zimehifadhiwa kidijitali. Vilevile, Wizara imejenga uzio wa ukuta katika Makumbusho ya Dkt. Rashid M. Kawawa, Bombambili (Songea) ili kuimarisha usalama wa mikusanyo.

**136. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeboresha vioneshwa katika Makumbusho kwa kujenga na kukarabati nyumba tano za jamii ya Wachaga, Waha, Wagogo, Wasambaa, Wanyambo, na Wafipa. Aidha, Shirika linakamilisha Mpango wa Matumizi ya Ardhi ya Kijiji cha Makumbusho Dar es Salaam. Mpango huo umeainisha maeneo ya mgahawa, ofisi, maonesho ya nyumba za asili na eneo la uwekezaji ambapo ujenzi wa mgahawa unaendelea.

**137. Mheshimiwa Spika,** Shirika limefanya utafiti katika Nyanja 20, ambapo 16 ni za utafiti wa mikusanyo iliyohifadhiwa kwenye makumbusho na nne kwenye Nyanja

za akiolojia, paleontolojia na biolojia. Utafiti kwenye Nyanja 13 za mikusanyo umeshirikisha watafiti wa nje kwa kushirikiana na watafiti wa Makumbusho ya Taifa. Utafiti katika Nyanja tatu za mikusanyo umefanywa na watafiti wa Makumbusho ya Taifa. Aidha, utafiti mmoja umefanywa kwenye Nyanja ya akiolojia na paleontolojia katika bonde la Olduvai na utafiti katika nyanja tatu za biolojia umefanyika kwenye Milima ya Usambara Mashariki. Matokeo ya utafiti yamesaidia kupata taarifa sahihi za kuweka kwenye maonesho ndani ya kumbi za makumbusho na kwa ajili ya kuboresha program za elimu.

**138. Mheshimiwa Spika**, Katika kuwajengea watumishi uwezo na kubadilishana uzoefu, wataalam wawili wamehudhuria mafunzo ya uhifadhi wa mikusanyo Ujerumani. Aidha, Shirika limeshirikiana na Makumbusho za mataifa ya Kenya na Uganda kufanya utafiti wa tathmini ya takwimu za anuai za vipepeo na nondo wachavushao Afrika Mashariki. Matokeo yanaonyesha kuwa idadi ya vipepeo hao inapungua. Hivyo, kuna umuhimu wa kuongeza jitihada za kuwahifadhi ili kuepusha janga la njaa.

**139. Mheshimiwa Spika**, Shirika limetoa elimu ya chimbuko la binadamu kwa walimu na wanafunzi wa shule za Sekondari za mikoa ya Arusha na Kilimanjaro. Warsha nane zilizojumuishwa walimu 144 zimefanyika ili kuwajengea uwezo wa kufundisha kuhusu Chimbuko la Binadamu Afrika. Aidha, jumla ya wanafunzi 458 kutoka Shule 15 za Sekondari wametembelea Makumbusho ya Elimu Viumbe - Arusha na kujifunza masuala ya Makumbusho.

#### **5.4.5 Miradi ya Maendeleo**

**140. Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2017/2018 jumla ya **Shilingi 51,803,284,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza miradi **12** ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 33,803,284,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 18,000,000,000** fedha za nje. Hadi mwezi Machi 2018, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 27,946,780,919** sawa na asilimia **54** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya hizo, **Shilingi 11,353,250,489** ni fedha za ndani na **Shilingi 16,593,530,813** fedha za nje. Utekelezaji wa Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

#### 5.4.5.1 Idara ya Sera na Mipango

##### i. Mradi wa Kusimamia Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini

**141. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Kusimamia Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini (Resilient Natural Resources for Tourism and Growth - REGROW) unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia. Kazi zilizotekelezwa ni kukamilisha Andiko la Usanifu (*Project Appraisal Document*); kuainisha shughuli zitakazotekelezwa; kusaini Mkataba; kufanya upembuzi yakinifu; kuandaa hadidu za rejea kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na uendelezaji utalii; na uzinduzi wa mradi.

#### 5.4.5.2 Idara ya Wanyamapori

##### i. Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ikolojia ya Ardhioevu ya Bonde la Mto Kilombero na Mto Rufiji

**142. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ikolojia ya Ardhioevu ya Bonde la Mto Kilombero na Mto Rufiji (*Kilombero and Lower Rufiji Wetlands Ecosystem Management Project - KILORWEMP*) unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Ubelgiji. Kazi zilizotekelezwa ni uperembaji katika Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori na kutayarisha mipango ya uvunaji wa misitu katika eneo la Mradi.

##### ii. Mradi wa Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi Ujangili

**143. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia fedha za ndani. Mradi unajumuisha ujenzi wa miundo mbinu katika Hifadhi za Taifa, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Mapori ya Akiba. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ukarabati wa barabara na ujenzi wa nyumba za watumishi ndani ya Hifadhi. Fedha zilizotumika kwa NCAA na TANAPA zimetokana na mapato ya ndani.

**iii. Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili**

**144. Mheshimiwa Spika,** Mradi unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali za Ujerumani na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Hifadhi ya Taifa Serengeti, Pori la Akiba Selous na Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro. Kazi zilizotekelezwa ni kutayarisha Mpango Mkakati wa TAWA, ununuzi wa vitendea kazi, na kutoa mafunzo kwa wataalam.

**5.4.5.3 Idara ya Misitu na Nyuki**

**i. Mradi wa Kujenga Uwezo wa Jamii katika Kusimamia Raslimali za Misitu kwa Tija na Misingi Endelevu**

**145. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Kujenga Uwezo wa Jamii katika Kusimamia Raslimali za Misitu kwa Tija na Misingi Endelevu (*Empowering communities through training on participatory forest management, REDD & Climate Change Initiative Program - CCIP*) unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali za Norway na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kutoa elimu kwa viongozi 294 wa vijiji na Jumuiya za Hifadhi za Jamii (CBO`s), kusimamia utekelezaji wa program ya MKUHUMI na Mabadiliko ya Tabianchi. Mradi huo umeboresha miundombinu ya Chuo cha Misitu Olmotonyi.

**ii. Mradi wa Panda Miti Kibiashara**

**146. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Panda Miti Kibiashara (*Support to Private Forest Plantations and Value Chains in Tanzania – PFP*) unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali za Finland na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Nyanda za Juu Kusini. Kazi zilizotekelezwa ni kuwezesha vikundi 120 kupanda jumla ya hektari 4,000 za miti ili kuwaongezea wananchi kipato na kuimarisha usawa wa kijinsia, kufanya utafiti kuhusu misitu binafsi, kuendesha mafunzo ya muda mfupi katika kituo cha mafunzo Mafinga na kuwezesha wanafunzi 30 kupata mafunzo VETA.

**iii. Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki**

**147. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki (*Capacity Building in Forestry and Beekeeping*) unatekelezwa kwa fedha za ndani kwa lengo la kuziwezesha taasisi za mafunzo na utafiti zilizo chini ya Idara ya Misitu na Nyuki kutekeleza majukumu yao. Baadhi ya kazi zilizotekelezwa ni kujenga maabara na kuboresha miundombinu ya taasisi za mafunzo za Chuo cha Misitu Olmotonyi, Chuo cha Viwanda vya Misitu, Chuo cha Mafunzo ya Nyuki na ujenzi wa Maabara ya Nyuki – TAWIRI.

**iv. Mradi wa Kuwezesha Wananchi Kunufaika na Raslimali za Misitu kwa Maendeleo ya Kiuchumi**

**148. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Kuwezesha Wananchi Kunufaika na Raslimali za Misitu kwa Maendeleo ya Kiuchumi (*Natural Resources Management for Local Economic Development - NRM/LED*) unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali za Ubelgiji na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya za: Uvinza, Kigoma, Kasulu, Kibondo, Kakonko, na Buhigwe. Kazi zilizotekelezwa ni upembuzi yakinifu wa maliasili na huduma za ikolojia na kuhamasisha uhifadhi wa misitu katika ngazi ya wilaya na mkoa.

**5.4.5.4 Idara ya Utalii**

**i. Miradi ya Utalii House Phase II na Theme Park**

**149. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Utalii House Phase II unahusu ujenzi wa jengo la pili la kitegauchumi katika eneo lililokuwa Ubalozi wa Marekani. Aidha, mradi wa Theme Park unahusu uendelezaji wa utalii katika Jiji la Dar es Salaam. Kupitia mradi huo, eneo maalum litatengwa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za utalii kama hoteli za kitalii; viwanja vya michezo; bustani za wanyamapori; kumbi za sinema na huduma nyingine za kijamii.

## **5.5 Masuala Mtambuka**

### **5.5.1. Utawala na Raslimaliwatu**

**150. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi 17 kwa kuwawezesha kupata mafunzo ya muda mfupi (3) na muda mrefu (14) ndani na nje ya nchi. Aidha, taasisi zimeendelea kuwawezesha watumishi kupata mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu na kuwapatia vitendea kazi. Vilevile, Wizara imeendelea kusimamia maslahi, maadili, ustawi na afya za watumishi ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wanaoishi na VVU na Ukimwi kupata lishe bora.

**151. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa majukumu yake katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji. Kazi hiyo imetekelezwa na viongozi wakuu wa wizara, wakurugenzi, wakuu wa vitengo na maafisa. Aidha, maeneo yaliyotembelewa yanajumuisha Hifadhi za Taifa, Hifadhi ya Ngorongoro, Mapori ya Akiba na Tengefu, Hifadhi za Misitu, maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMAs), maeneo ya malikale na shughuli za utalii. Kupitia tathmini iliyofanyika, Wizara imeibua masuala ambayo yanahitaji kuboreshwa ili kuendeleza sekta ya maliasili na utalii.

### **5.5.2. Kuanzisha Jeshi Usu**

**152. Mheshimiwa Spika,** Wizara imedhamiria kupunguza tatizo sugu la ujangili wa wanyamapori na misitu kwa kuboresha mfumo wa utendaji kazi kutoka wa kiraia kwenda Jeshi Usu (Paramilitary). Lengo la mfumo huo ni kuimarisha ulinzi wa maliasili za taifa ikiwa ni pamoja na kukabiliana na changamoto za ujangili unaotumia mbinu za kisasa ikiwa ni pamoja na silaha za kivita. Kufuatia azma hiyo ya Serikali, Wizara inafanya marekebisho ya muundo wa kiutendaji wa mashirika ya TANAPA, NCAA, TAWA na TFS. Aidha, Wizara inaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wa taaluma za wanyamapori, misitu na nyuki. Hadi Machi 2018, watumishi 678 wa Sekta ndogo za Wanyamapori (505) na Misitu (173) wamepatiwa mafunzo. Vilevile, Wizara inaendelea kujenga uwezo kitaasisi kwa kuongeza vitendea kazi na matumizi ya teknolojia.

### 5.5.3. Mifumo na Matumizi ya TEHAMA

**153. Mheshimiwa Spika,** Hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi wa Bunge la 11 pamoja na mambo mengine ilisisitiza kuhusu kuboresha na kudhibiti ukusanyaji mapato. Kwa kuzingatia maelekezo hayo, Wizara imeanza kutengeneza mfumo mmoja funganishi wa TEHAMA unaoitwa “**MNRT Portal**” wa kutoa leseni na vibali, ukusanyaji wa takwimu na mapato kutoka vyanzo mbalimbali vya sekta ya maliasili na utalii. Mfumo huo ambao utaunganishwa na mfumo wa Serikali wa malipo wa Ki-elektronik - *Government electronic Payment Gateway* (GePG) na kuhuishwa na mifumo mingine ya Serikali kama vile, ya Uhamiaji, NIDA, TIRA, BRELA, TRA, na NBS utaiwezesha Wizara: kufuatilia watalii wa nje na wa ndani; kukusanya na kuchambua takwimu za sekta ya maliasili na Utalii kwa wakati; kuimarisha utoaji wa huduma kwa wateja; na kufanikisha ukusanyaji na udhibiti wa mapato. Mfumo huo ambao utatumiwa na Wizara, Taasisi na wadau utaanza kutumika rasmi mwa mwaka ujao wa fedha.

### 5.5.4. Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

**154. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza mikataba ya East African Community (EAC), Southern African Development Community (SADC), Convention on International Trade in Endangered Species of Wild Fauna and Flora (CITES), United Nations - World Tourism Organisation (UNWTO), United Nations Development Programme (UNDP), United Nations Educational, Scientific and Cultural Organisation (UNESCO), International Council of Museums (ICOM), International Center for the Study of the Preservation and Resoration of Cultural Property (ICCROM), International Council on Monument and Sites (ICOMOS), na Lusaka Agreement Task Force (LATF) katika kutekeleza majukumu yake.

**155.** Kupitia ushirikiano huo, Wizara inanufaika na misaada ya kitaalam na fedha, kubadilishana uzoefu, kupata vifaa mbalimbali na kuimarisha ushirikiano. Kutokana na uanachama huu, Wizara imetekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na: ujenzi wa miundo mbinu; uendelezaji utalii; kuboresha maisha ya jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi; kubadilishana uzoefu katika uhifadhi na uendelezaji utalii.

### 5.5.5. Utatuzi wa Migogoro

**156. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyotoa Novemba 2016 kuhusu kuweka vigingi vya mipaka kwenye maeneo ya hifadhi ili kuepuka migogoro. Hadi Machi 2018, jumla ya vigingi 27,942 vimesimikwa ikiwa ni sawa na asilimia 79.4 ya malengo. Kazi hiyo inatekelezwa na TANAPA, NCAA, TAWA, na TFS kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Ofisi ya Rais TAMISEMI; na wananchi. Maeneo yanayohusika ni Hifadhi za Taifa, Hifadhi ya Ngorongoro, Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu, na Hifadhi za Misitu.

**157. Mheshimiwa Spika**, Mnamo tarehe 6 Desemba 2017, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alielekeza Wizara ya Maliasili na Utalii kuunda chombo maalum kitakachosimamia eneo la Pori Tengefu Loliondo kwa maslahi mapana ya uhifadhi, maendeleo ya wananchi, wawekezaji wa shughuli za utalii na maendeleo ya sekta nyingine muhimu za kiuchumi bila migongano. Aidha, Mheshimiwa Waziri Mkuu alielekeza Wizara nyingine za kisekta zinazohusika zishiriki kikamilifu katika hatua zote za utekelezaji wa maelekezo hayo.

**158. Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia maelekezo ya Waziri Mkuu, Wizara imeandaa rasimu ya “Mkakati wa Usimamizi wa Pori Tengefu Loliondo” ambao umezingatia maslahi ya uhifadhi, maendeleo ya wananchi na ukuaji wa uchumi. Mkakati huo umewasilishwa kwenye kikao cha Mawaziri wa Wizara za kisekta zinazohusika na Pori Tengefu Loliondo kwa ajili ya maboresho. Kwa sasa, Wizara inakamilisha mapendekezo yaliyotolewa katika kikao hicho ambayo yatawasilishwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maelekezo yake. Sambamba na hatua hii, kila Wizara ya kisekta imewasilisha mapendekezo ya mwongozo wa utekelezaji wa majukumu ya kisekta kwenye eneo la Pori Tengefu Loliondo. Vilevile, majukumu yatakayotekelezwa na kila Wizara ya Kisekta yamezingatiwa katika mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019.

## **5.6 Majukumu ya Kimkakati**

### **5.6.1. Kutekeleza Agizo la Serikali la kuhamia Dodoma**

**159. Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza Agizo la Serikali la kuhamia Dodoma, Wizara imewahamisha watumishi 201. Aidha, Usanifu wa majengo na nyumba za baadhi ya watumishi umefanyika. Wizara imepata ofisi mbili ambapo watumishi wanatumia Ofisi ya Chuo Kikuu Dodoma (University of Dodoma – UDOM) na Ofisi iliyopo eneo la Kilimani Barabara ya Askari. Watumishi 46 waliobakia Ofisi ya Dar es Salaam watahamia katika mwaka wa fedha 2018/2019.

### **5.6.2. Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Rufiji**

**160. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa kuzalisha umeme Rufiji (*Rufiji Hydropower Project - Stigler's Gorge*) unatekelezwa na Wizara ya Nishati, ambapo eneo la mradi liko katika Pori la Akiba Selous. Katika utekelezaji wa Mradi huu, Wizara ya Maliasili na Utalii imepewa jukumu la kukata miti katika eneo ambapo bwawa hilo litajengwa. Aidha, Wizara imepewa jukumu la kuimarisha ulinzi wa maeneo ya lindimaji na kutoa wataalam kwenye eneo la Mradi. Katika mwaka huu wa fedha, Wizara imeanza kufanya tathmini ya maliasili zinazopatikana kwenye eneo la Mradi. Tathmini hiyo inalenga kupata thamani ya mazao ya misitu yatakayovunwa na kuuzwa kibiashara na kutambua spishi za mimea na wanyamapori zinazoweza kuwa hatarini kutoweka ili kuweka mikakati ya kuzihifadhi. Majukumu hayo ya Wizara yanatekelezwa kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania. Vilevile, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania inashiriki katika kufanya tathmini ya athari za kimazingira.

### **5.6.3. Kuwezesha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji kwenye Sekta**

**161. Mheshimiwa Spika**, Wizara katika ripoti ya “Ease of Doing Business” inayoandaliwa na Benki ya Dunia, inahusika na viashiria vya Uanzishwaji na Uendeshwaji wa Biashara na Taratibu za Kusafirisha bidhaa na huduma nje ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imehusika katika kuandaa Mpango kazi wa

Kitaifa wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (*Comprehensive Action Plan for Improvement of Business Environment and Investment Climate*). Katika kurahisisha mazingira ya kufanya biashara nchini, Wizara inaendelea kupitia sera, sheria na kanuni za usimamizi wa maliasili, malikale na uendelezaji utalii.

## **5.7 Mafanikio, Changamoto na Utatuzi Wake**

### **5.7.1 Mafanikio**

**162. Mheshimiwa Spika**, Wizara imefanikiwa kupunguza matukio ya ujangili, biashara haramu ya misitu na wanyamapori, uvamizi wa maeneo ya hifadhi na matukio ya moto. Mafanikio haya yamechangiwa hasa na uimarishaji wa mipaka ya hifadhi, ulinzi na intelijensia, na ushirikishaji wananchi na wadau wengine katika uhifadhi.

**163. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017, idadi ya watalii walioingia nchini imeongezeka kutoka watalii 1,284,279 (mwaka 2016) hadi kufikia watalii 1,327,143 (mwaka 2017). Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 3.3. Watalii kutoka Marekani wameongoza katika kuitembelea Tanzania wakifuatiwa na nchi za Uingereza, India, Uholanzi na Uswisi. Aidha, mapato yatokanayo na Utalii yameongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 2,131.57 (mwaka 2016) hadi kufikia Dola za Marekani milioni 2,250.3 (mwaka 2017). Ongezeko hilo la mapato ni sawa na asilimia 5.6.

**164. Mheshimiwa Spika**, Mafanikio hayo yanatokana na ujenzi wa miundombinu ya barabara, kuongezeka kwa kasi ya kuboresha na kutangaza vivutio vya utalii; kuimarishwa kwa mifumo ya ukusanyaji maduhuli; na kudhibiti matukio ya ujangili na matumizi yasiyo endelevu ya maliasili na malikale.

### **5.7.2 Changamoto**

**165. Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujangili na biashara haramu ya nyara za Serikali; uvamizi wa maeneo ya hifadhi kwa shughuli za kilimo, ufugaji na makazi;

kuzuiwa kwa maeneo ya shoroba na mapito ya wanyamapori (*wildlife corridors/migratory routes*) mazalia (*breeding areas*) na mtawanyiko (*Dispersal areas*). Aidha, matatizo ya moto, ongezeko la uchimbaji wa madini ndani ya maeneo ya uhifadhi na ukataji miti kwa ajili ya biashara ya mkaa, ujenzi na matumizi mengineyo yameendelea kuathiri sehemu kubwa ya misitu. Vilevile, miundombinu hususan barababara, maji, umeme, viwanja vya ndege (*airstrips*) na njia za mawasiliano katika maeneo ya hifadhi na malikale hairidhishi. Pia, mwamko wa wananchi kushiriki katika utalii wa ndani na uelewa wa jamii na wadau kuhusu thamani na umuhimu wa malikale ni mdogo.

**166. Mheshimiwa Spika,** Athari za kutohifadhi vema maliasili na mazingira zinajitokeza katika kupungua kwa mtiririko wa maji na kukauka kwa baadhi ya vyanzo vya maji. Kwa mfano, mito ya Pangani, Ruaha, Rufiji, Ruvu, Mara, Simiyu, Kilombero, Malagarasi, Kagera, Moyowosi na Ruvuma. Aidha, kwenye baadhi ya maeneo kumekuwepo na upungufu wa maji kwa shughuli za kilimo, mifugo, wanyamapori, nyumbani na viwandani. Vilevile, kumekuwepo na milipuko ya magonjwa yanayoambukizwa kutokana na muingiliano wa binadamu, mifugo na wanyamapori. Kwa mfano, magonjwa ya kimeta (*anthrax*), kichaa cha mbwa (*rabies*) na homa ya vipindi (*brucellosis*). Pia, kutokana na miundo mbinu hafifu, imekuwa vigumu kwa baadhi ya vivutio vya utalii kufikika. Sanjari na hilo, uelewa mdogo wa jamii na wadau kuhusu malikale kumesababisha maeneo hayo kutoendelezwa ipasavyo.

**167. Mheshimiwa Spika,** Kutokana na changamoto hizo, Wizara itaendelea kuchukua hatua stahiki wakati wa kutekeleza Mpango na Bajeti ya mwaka 2018/2019. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha uhifadhi wa maliasili, malikale na kuendeleza utalii; kubadili mifumo ya usimamizi; kuimarisha ushirikiano na Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya na Mikoa; ushirikishaji wa vyombo na Mamlaka nyingine za Serikali. Aidha, Wizara itaendelea kuwashirikisha wananchi na wadau wengine, hususani sekta binafsi, Washirika wa Maendeleo, Asasi za Kiraia na marafiki wa uhifadhi katika kutekeleza majukumu yake.

### 5.7.3 Utatuzi wa Changamoto

**168. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kutumia mikakati mbalimbali katika kutatua changamoto za usimamizi wa maliasili na malikale na kuendeleza utalii. Mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha mifumo ya usimamizi; kuimarisha ushirikishaji wadau; kuendelea kutoa elimu na kuwahamasisha wananchi; kuandaa na kutekeleza mikakati ya upandaji miti na ufugaji nyuki; kutatua migogoro kwa njia shirikishi; kuongeza wigo wa mazao ya utalii; kuimarisha utangazaji wa vivutio vya utalii; kudumisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa; na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji maduhuli.

## 6.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**169. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara itatekeleza mpango na bajeti ambao umezingatia majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Sehemu ya Pili ya Hotuba hii. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza majukumu ya Taifa ya Kimkakati na maagizo mbalimbali ya Serikali ikiwa ni pamoja na kuzingatia mikakati ya kutatua changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2017/2018.

### 6.1. Ukusanyaji Maduhuli

**170. Mheshimiwa Spika**, Wizara na Taasisi zake inakadiriya kukusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 63.2** kutokana na vyanzo vya Idara na Taasisi zilizo chini yake. Kiasi hicho kitakusanywa na Wizara (**Shilingi Bilioni 23.6**), Taasisi zinazopata Ruzuku kupitia Wizara (**Shilingi Bilioni 24.7**), na Mfuko wa Uhifadhi wa Wanyamapori Tanzania (TWPF) na Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF) (**Shilingi Bilioni 14.8**).

**171. Mheshimiwa Spika**, Mashirika yaliyochini ya Wizara (TANAPA, NCAA, TAWA, na TFS) yanakadiriya kukusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 623.5** Kiasi hicho kitakusanywa na TANAPA (**Shilingi Bilioni 292.8**), NCAA (**Shilingi Bilioni 156.6**), TAWA (**Shilingi Bilioni 47.5**) na TFS (**Shilingi Bilioni 126.6**). Mashirika haya

hukusanya maduhuli kwa ajili ya matumizi yao na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

## **6.2. Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

**172. Mheshimiwa Spika**, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi Bilioni 115.8** kwa Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni 85.8** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi Bilioni 30** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Utekelezaji wa majukumu ya wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 umefafanuliwa kama ifuatavyo:-

## **6.3. Mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni**

**173. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Misitu (1998), Ufugaji Nyuki (1998) na Utalii (1999). Kazi hii itatekelezwa sanjari na kutayarisha Mikakati ya Utekelezaji wa Sera hizo. Aidha, Wizara itaendelea kupitia Sheria za Usimamizi wa Maliasili, Malikale na Utalii kwa lengo la kuondoa migongano ya kisheria, kutambua wajibu wa wadau na kuimarisha usimamizi. Vilevile, Wizara itaendelea kukamilisha mapitio ya Kanuni za Biashara ya Nyara; na usimamizi wa Mkataba wa CITES.

## **6.4. Kazi Zitakazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake**

### **6.4.1. Sekta Ndogo ya Wanyamapori**

#### **6.4.1.1. Idara ya Wanyamapori**

**174. Mheshimiwa Spika**, Wizara itahakiki na kukusanya nyara zilizopo katika vituo vya Polisi, Halmashauri za Wilaya, Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro; na kukarabati na kuweka vifaa vya kisasa vya ulinzi katika ghala la nyara (*Ivory room*) lililopo Dar es Salaam. Aidha, Wizara itaendelea kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathirika na wanyamapori wakali na waharibifu. Vilevile, Wizara itakamilisha taratibu za kuanzisha Mapori mawili ya

Akiba (Litumbandyosi na Gesimasowa - Ruvuma) na kupandisha hadhi WMA ya Wami-Mbiki kuwa Pori la Akiba.

#### **6.4.1.2. Shirika la Hifadhi za Taifa**

**175. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Hifadhi za Taifa litaendelea kutekeleza jukumu lake la uhifadhi na kuendeleza utalii. Katika uhifadhi, Shirika litaendelea kurejesha uoto wa asili na mazingira yaliyoharibiwa katika hifadhi za Katavi, Kilimanjaro, Saadani na Ruaha. Aidha, miundombinu ya kuhifadhi maji wakati wa kiangazi itawekwa katika Hifadhi za Taifa Serengeti, Mkomazi, Mikumi, Katavi na Saadani. Vilevile, awamu ya kwanza ya uwezeshaji wa kutayarisha mipango ya matumizi bora ya ardhi itatekelezwa katika vijiji 95 kati ya 392 vinavyopakana na Hifadhi za Taifa Ruaha, Kitulo, Mikumi, Mkomazi, Serengeti na Kilimanjaro. Pia, vituo vya askari (*ranger posts*) vine vitajengwa kwenye maeneo yenye matukio ya mara kwa mara ya wanyamapori wakali na waharibifu, hususan, Bunda, Tarime, Itilima na Serengeti. Aidha, Shirika litajiimarisha katika kudhibiti ujangili kwa kufanya doria na kukamilisha taratibu za kuingia kwenye mfumo wa jeshi-usu.

**176. Mheshimiwa Spika,** Kupitia utalii, Shirika linatarajia kupokea watalii 1,141,462 kati yao 715,314 ni wa watalii wa nje na 426,148 kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Shirika litaanza kutekeleza mkakati wa kuendeleza vivutio vya kihistoria na kitamaduni vilivyo jirani na hifadhi za Taifa. Kupitia mkakati huo, huduma za utalii ikiwemo usafiri wa anga, majini na barabara ndani ya hifadhi zitaboreshwa. Aidha, vituo vya malikale na hifadhi za taifa vitatangazwa kwa pamoja ili kuongeza wigo wa vivutio vya utalii, uelewa na mvuto kwa wageni, na hatimaye kuongeza siku wanazokaa nchini na mapato.

#### **6.4.1.3. Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro**

**177. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro itaendelea kuboresha mtandao wa miundombinu ya barabara ikiwemo ujenzi wa barabara ya Loduare hadi Golini yenye urefu wa kilomita 88 kwa kiwango cha lami; kukarabati viwanja vya ndege; kuboresha shughuli za utalii na mifumo ya malipo ya huduma za

utalii. Aidha, Mamlaka itaongeza wigo wa shughuli za utalii kama safari za maputo ya joto (*hot air balloons*) na uendeshaji wa baiskeli ili kuongeza idadi ya siku wanazokaa watalii.

**178. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka itaendelea kuimarisha shughuli za ulinzi wa eneo la hifadhi ikiwa ni pamoja na kujenga vituo viwili vya askari kwenye maeneo yenye changamoto za kiusalama, kununua vifaa vya kisasa vya ulinzi na kuongeza mafunzo kwa Askari. Aidha, Mamlaka itaandaa Mpango Mkakati wa Kuendeleza Mifugo (*Livestock Development Strategy*) katika eneo la Hifadhi. Vilevile, Mamlaka itaendelea kutoa huduma za jamii kwa wenyeji katika nyanja za elimu, afya, maji, chakula na miradi mingine ya maendeleo.

#### **6.4.1.4. Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania**

**179. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania, itaendesha doria za kawaida siku doria 188,029 na za anga kwa saa 900 katika Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu. Aidha, mafunzo kwa watumishi 44 wa Kitengo cha Mbwa na Timu ya Kushughulikia Matukio kwa Haraka (*Rapid Response Team*) na watumishi 220 kuhusu Jeshi Usu yatatolewa. Vilevile, mafunzo ya uendeshaji wa mashtaka yatatolewa kwa watumishi 20 na askari 20 wa Vijiji watafundishwa mbinu za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu. Pia, elimu ya uhifadhi wa wanyamapori itatolewa kwa jamii iliyopo jirani na Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu.

**180. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka itafanya tathmini na kulipa fidia kwa wananchi wanaoishi ndani ya Pori la Akiba Mkungunero. Kazi nyingine zitakazofanyika ni pamoja na: i) kuweka umeme katika ofisi za Mapori ya Akiba Selous, Lukwika-Lumesule na Kijereshi; na ii) kuboresha mtandao wa barabara zenye urefu wa kilomita 1,192 katika Mapori ya Akiba Selous (596 km), Maswa (99 km), Mpanga – Kipengele (17 km), Burigi - Biharamulo – Kimisi (368 km), Kijereshi (53 km) na Swagaswaga (59 km). Aidha, Mamlaka itajenga ofisi katika Pori la Akiba Liparamba na Swagaswaga; na kukarabati nyumba tano, vyoo nane na ofisi mbili Makao makuu ya Mamlaka na vituo 14 (6 KDU na nane Mapori ya Akiba).

**181. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka itajenga ofisi ya walimu katika Shule ya Sekondari Mwaseni, Rufiji. Aidha, maghala 18 ya silaha yatajengwa katika vituo mbalimbali na vituo vitatu vya askari wanyamapori vitajengwa Dodoma, Tunduru na Nzega ili kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo hayo. Vilevile, bwawa la kijiji cha Itaswi lililoko jirani na Pori la Akiba Mkungunero litakarabatiwa ili kuwezesha wananchi kupata chanzo mbadala cha maji.

**182. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka itaendelea kukamilisha Mkakati wa Uwekezaji kwenye maeneo ya hoteli, loji na kambi za kulala wageni. Utekelezaji wa Mkakati huo utashirikisha sekta binafsi. Hatua hiyo inalenga kuongeza wigo wa mazao ya utalii na kuongeza idadi ya watalii na mapato.

#### **6.4.1.5. Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania**

**183. Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania itaendelea kufanya, kuratibu na kusambaza matokeo ya miradi 126 ya utafiti wa wanyamapori. Miradi hiyo imejikita kwenye ikolojia, tabia za wanyamapori, mwenendo wa magonjwa, ufugaji nyuki, na migongano kati ya binadamu na wanyamapori. Aidha, Taasisi itatengeneza na kusambaza mizinga 1,500 kwa wadau na kukamilisha ujenzi wa maabara ya kisasa ya ufugaji nyuki. Vilevile, Taasisi itafanya sensa ya wanyamapori katika mfumo ikolojia wa Selous-Mikumi na sensa ya mamba na viboko katika maeneo mengine.

#### **6.4.1.6. Vyuvo vya Taaluma ya Wanyamapori**

**184. Mheshimiwa Spika**, Vyuvo vya Taaluma ya Wanyamapori vitaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wanafunzi 1,021 na muda mfupi kwa wanafunzi 720. Katika Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka, wanafunzi 560 watapata mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Astashahada, Stashahada na Shahada; na waongoza watalii wa mlimani 400 watapata mafunzo ya muda mfupi. Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi itatoa mafunzo ya muda mrefu ngazi ya Astashahada kwa wanafunzi 441 na mafunzo ya muda mfupi kwa wanafunzi 200.

Aidha, Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii – Likuyu Sekamaganga kitatoa mafunzo ya muda mrefu ngazi ya Astashahada kwa wanafunzi 20 na muda mfupi wanafunzi 120 ambao ni Askari Wanyamapori wa Vijiji na Viongozi wa Kamati za Maliasili za Vijiji.

**185. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka kitaanza kujenga jengo moja la mafunzo litakalokuwa na vyumba vinne vya mihadhara, ukumbi wa mikutano na ofisi sita za wahadhiri. Aidha, Chuo kitanunua gari moja kwa ajili ya kuwezesha mafunzo kwa vitendo. Vilevile, Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi itaandaa kanuni za uendeshaji wa Taasisi; kupitia mitaala ya mafunzo na Mpango Mkakati; kuandaa Mpango wa Biashara wa Taasisi; kujenga nyumba mbili za watumishi; na kununua mahema 20. Pia, Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii – Likuyu Sekamaganga kitakamilisha taratibu za usajili NACTE na kuanzisha kozi ya Astashahada ya awali ya waongoza watalii.

#### **6.4.1.7. Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania**

**186. Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania utaendelea kuwezesha Kikosi Maalum cha Taifa cha Kupambana na Ujangili katika kutekeleza majukumu yake; kuwezesha mapitio ya kanuni mbalimbali, usimamizi wa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori na kuwezesha kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu.

#### **6.4.2. Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki**

##### **6.4.2.1. Idara ya Misitu na Nyuki**

**187. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kuratibu siku za kitaifa za kupanda miti na kutundika mizinga; kuzijengea uwezo Kamati za Usimamizi wa Misitu za Vijiji na kuratibu mikutano minne ya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Misitu (NAFAC).

#### 6.4.2.2. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania

**188. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania unatarajia kupanda miti kwenye mashamba yenye ukubwa wa jumla ya hektari 9,683. Aidha, Wakala utaongeza upandaji miti kwenye jumla ya hektari 1,550 kwenye mashamba mapya ya miti ya Wino (Songea), Iyondo Msimwa (Ileje), Biharamulo (Chato), Mpepo (Nyasa), Buhigwe (Kigoma) na Mtibwa/ Pagale (Mvomero). Aidha, Wakala utawezesha wananchi kuotesha na kupanda miche ya miti 8,481,000 katika vijiji vinavyozunguka hifadhi za misitu na mashamba ya miti. Vilevile, Wakala utakarabati barabara za msituni zenye urefu wa kilomita 1,869 na kujenga kilomita 189 za barabara.

**189. Mheshimiwa Spika,** Wakala utatayarisha mipango 57 ya usimamizi wa hifadhi za misitu, mikoko, nyuki na mashamba ya miti. Aidha, Wakala utaendelea kuimarisha mipaka ya hifadhi za misitu kwa kusafisha mipaka yenye kilomita 10,546.57, kusimika vigingi 3,318, kuweka mabango 1,601 ya tahadhari na kuchimba mashimo mwelekeo. Vilevile, jumla ya mita za ujazo 817,964 kutoka katika mashamba ya miti zitauzwa kwa wadau wanaostahili ikiwa ni pamoja na vijiji vilivyopo karibu na mashamba hayo.

**190. Mheshimiwa Spika,** Wakala utaboresha miundo mbinu na vitendea kazi kwenye misitu ya hifadhi ya mazingira asilia ili kuimarisha utalii ikolojia. Kazi zitakazofanyika ni: kusafisha kilomita 193 za njia asili (*Nature trails*) na kilomita 147.5 za njia vinjari (*drive routes*); kujenga kambi 18 za kupumzika wageni na kuendeleza maeneo mengine matano ya shughuli za utalii (*recreational sites*). Aidha, hatua za kupandisha hadhi hifadhi za misitu ya Kalambo (Kalambo), Mwambes (Tunduru), Itulu (Sikonge) na Uvinza (Uvinza) zitakamilishwa; na kukarabati ofisi sita, kuendeleza ujenzi wa nyumba tisa za watumishi na kujenga nyumba 15 za ulinzi katika mashamba ya miti na misitu ya hifadhi ya mazingira asilia. Vilevile, mfumo wa maji safi utakarabatiwa katika vituo 28 vya mashamba ya miti na misitu ya hifadhi, kujenga ofisi 13 na kununua viwanja 19, magari 19, pikipiki 53, jenereta 25, trekta mbili na boti saba.

**191. Mheshimiwa Spika,** Wakala utafanya doria katika mashamba ya miti na Misitu ya hifadhi. Aidha, ukaguzi wa miti ya mbao yenye mita za ujazo 827,266 na miti ya kuni yenye mita za ujazo 18,900 utafanyika. Vilevile, mikutano ya kampeni za uhamasishaji wa kuepuka madhara ya moto itafanyika kwenye vijiji 538 vinavyozunguka mashamba ya miti na Misitu ya hifadhi.

**192. Mheshimiwa Spika,** Wakala utaendelea kusimamia manzuki (apiaries) 143 zenye jumla ya mizinga 6,214; kuanzisha sehemu mbili za kuchakata na kuhifadhi asali; kupanda mazao yanayotoa maua kwenye maeneo ya manzuki; kuwapatia mafunzo wananchi 90; na kutoa mizinga 173 kwa wafugaji nyuki. Wakala utawezesha kutangazwa kwa manzuki mbili kwa kushirikisha Halmashauri za Wilaya. Aidha, asali itaendelea kufanyiwa uchambuzi wa kimaabara ili kuhakiki ubora wake na kuendelea kuuza katika soko la ndani na nje ya nchi.

#### **6.4.2.3. Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania**

**193. Mheshimiwa Spika,** Wakala utazalisha na kuuza miche 4,600,000 ya miti; na utakusanya tani 25 za mbegu bora za miti na kuuza tani 20. Aidha, Wakala kwa kushirikiana na Mfuko wa Misitu Tanzania utaanzisha bustani ya miti yenye uwezo wa kuzalisha miche 1,000,000 mjini Dodoma kwa ajili ya mahitaji ya Jiji la Dodoma na viunga vyake.

**194. Mheshimiwa Spika,** Wakala utafanya majaribio ya namna ya kukusanya na kuhifadhi aina nane za mbegu za miti, kuainisha vyanzo 10 vya mbegu kati ya 360 kutoka misitu ya hifadhi na mashamba. Aidha, vyanzo vitano vya mbegu bora za miti vitaanzishwa ikiwemo vyanzo vya miti iliyo katika hatari ya kutoweka.

#### **6.4.2.4. Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania**

**195. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania itaanzisha majaribio ya kiutafiti ya upandaji sahihi wa miti kwenye eneo la jumla ya hektari 100 katika Kanda za Ziwa, Kati, Mashariki, Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini; na kusimamia majaribio mapya ya utafiti. Matokeo ya majaribio haya yataongeza wigo

wa spishi za miti ya asili itakayokuwa na uwezo wa kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Taasisi itaendelea na utafiti wa njia mbadala za kuzalisha miti bora ya kigeni na ya asili kwa kutumia vikonyo (*cuttings*) na tishu (*tissue culture*) katika vitalu vilivyopo Morogoro, Kwamarukanga (Korogwe) na Kongowe (Kibaha).

**196. Mheshimiwa Spika,** Taasisi itaendelea kufuatilia matukio ya moto kwenye misitu kwa kutumia vifaa vya kisasa na kutoa taarifa za uwepo wa wadudu na magonjwa yanayoshambulia miti na jinsi ya kukabiliana nayo. Aidha, utafiti wa kubaini athari za mabadiliko ya tabianchi katika uhifadhi na uendelezaji wa misitu utafanyika. Vilevile, Taasisi itafanya utafiti kuhusu teknolojia sanifu za kuchakata na kuongeza thamani ya mazao ya Misitu.

#### **6.4.2.5. Vyuvo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki**

**197. Mheshimiwa Spika,** Vyuvo vya Misitu na Ufugaji Nyuki vitaendelea kutoa mafunzo kwa kudahili jumla ya wanafunzi 1,254 kwenye Chuo cha Misitu Olmotonyi (800); Chuo cha Viwanda vya Misitu (204); na Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (250). Aidha, Chuo cha Viwanda vya Misitu, Moshi kitakamilisha jengo la maktaba na maabara.

#### **6.4.2.6. Mfuko wa Misitu Tanzania**

**198. Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Misitu Tanzania utawezesha miradi 294 inayoendelea na miradi mipya 62 ya uhifadhi, uendelezaji na usimamizi wa raslimali misitu. Miradi hiyo inajumuisha Mradi maalum wa kuanzisha shamba la miti ya kupandwa lenye ukubwa wa hektari 200 katika eneo la Ziwani – Mtwara. Aidha, Mfuko utaendelea kuwezesha uchapishaji wa majarida mawili: Misitu ni Mali na Jarida la Utafiti wa Misitu.

**199. Mheshimiwa Spika,** Mfuko utawezesha utoaji elimu kuhusu umuhimu wa uhifadhi, uendelezaji na matumizi endelevu ya raslimali misitu kupitia vyombo vya habari; huduma za ugani kwa kununua magari nane na

utayarishaji wa kanzidata. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni kununua vifaa vya maabara ya mbegu za miti TTSA; kukamilisha jengo la maktaba na maabara katika Chuo cha FITI na ukabarati wa jengo la utawala la Chuo cha Ufugaji Nyuki – Tabora. Aidha, Mfuko utawezesha ununuzi wa mashine ya kuchakata asali na vifaa vingine kwa ajili mafunzo kwa vitendo ya katika Chuo cha BTI – Tabora. Vile vile, Mfuko utawezesha ujenzi wa miundombinu na nyumba nne katika mashamba mapya ya miti ya Biharamulo, Mpepo, Iyondomsimwa, Pagale na Buhigwe.

### **6.4.3. Sekta Ndogo ya Utalii**

#### **6.4.3.1. Idara ya Utalii**

**200. Mheshimiwa Spika,** Katika kuboresha huduma za utalii, Wizara itaendelea kufanya ukaguzi wa wakala wa biashara za utalii katika kanda nne; na kuweka huduma za malazi katika daraja la nyota katika mikoa ya Kilimanjaro, Tanga na Mwanza. Kazi nyingine zitakazofanyika ni kutoa elimu kwa wakala wa biashara ya utalii katika kanda nne za utalii kuhusu Sheria, Kanuni na Miongozo ya uendeshaji wa biashara ya utalii; na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watoa huduma 500 katika fani ya utalii na ukarimu wakiwemo wale wanaokutana na mgeni moja kwa moja. Aidha, katika kupanua wigo na mazao ya utalii, Wizara itabainisha vivutio vipya vya utalii katika mikoa ya Simiyu, Geita, Kigoma, Kagera, Tanga na Manyara na kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi na Uendelezaji wa maeneo ya fukwe.

#### **6.4.3.2. Bodi ya Utalii Tanzania**

**201. Mheshimiwa Spika,** Katika juhudi za kutangaza utalii, Wizara itaendelea kuitambulisha Tanzania Kimataifa (*Destination Branding*) kwa lengo la kuvutia wageni wa kimataifa kutembelea vivutio vya utalii. Aidha, Wizara itakamilisha uanzishwaji wa “*Studio*” ya kuutangaza utalii kwa njia ya TEHAMA.

**202. Mheshimiwa Spika,** Bodi itaendelea kuweka mabango makubwa katika Majiji ya Dar es Salaam, Arusha, Moshi, Mwanza na Dodoma na maeneo ya kimkakati hususan viwanja vya ndege vya kimataifa, maeneo ya hoteli kubwa za kitalii, mipakani na viwanja vya michezo. Aidha, Bodi itakamilisha Mkakati wa Kukuza Utalii wa Mikutano katika jitihada za kupanua wigo wa mazao ya utalii. Vilevile, Bodi kwa kushirikiana na sekta binafsi itapitia Mkakati wa Utangazaji Utalii (2012-2017) ili kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi, kiteknolojia na kijamii.

#### **6.4.3.3. Chuo cha Taifa cha Utalii**

**203. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kuimarisha uendeshaji wa Chuo cha Taifa cha Utalii kwa kuhakikisha kinapata vitendea kazi na walimu wenye weledi. Aidha, Chuo kitadahili wanafunzi 215 wa Astashahada, 100 wa Stashahada na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 800. Vilevile, Chuo kwa kushirikiana na Chuo kikuu cha Vancouver, Kanada kitakamilisha mitaala ya shahada katika fani ya utalii na ukarimu. Mafunzo hayo yanatarajia kuanza kutolewa mwaka 2019/2020. Pia, Chuo kitaendelea kuboresha miundombinu ya majengo katika Kampasi za Temeke, Bustani na Arusha.

#### **6.4.4. Sekta Ndogo ya Mambo ya Kale**

##### **6.4.4.1. Idara ya Mambo ya Kale**

**204. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kupima maeneo manne ya malikale katika vituo vya Mtwaa Mkwawa - Kalenga na Zana za Mawe - Isimila (Iringa); Mapango ya Amboni (Tanga); na Magofu ya Kaole - Bagamoyo (Pwani). Vilevile, itahuisha orodha ya maeneo ya malikale katika mikoa ya Kanda ya Kusini; itabainisha na kuweka kumbukumbu ya majengo ya kihistoria katika Jiji la Dar es salaam; itajenga kituo cha kumbukumbu na taarifa katika eneo la Mapango ya Amboni na ofisi katika eneo la Engaruka. Pia, Wizara itakarabati Ofisi katika vituo vya Kilwa, Kituo cha Kumbukumbu na Taarifa (Kolo); na itaendelea kuelimisha wadau kuhusu umuhimu wa malikale. Aidha, Wizara itanunua boti kwa ajili ya kituo cha Kilwa na kuwezesha ukarabati wa magofu ya Kua - Mafia.

**205. Mheshimiwa Spika,** Kuhusu Nyumba Kumbukizi ya Mwalimu Nyerere (Magomeni – Dar es Salaam), Wizara itakarabati nyumba na kukusanya taarifa za kina kuhusu historia ya mwalimu na nyumba yake, kuboresha maonesho na kujenga ofisi za wafanyakazi.

**206. Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Mambo ya Kale utawezesha uboreshaji wa miundombinu na utafiti. Kazi zitakazofanyika ni: ujenzi wa vituo vya Mbozi - Songwe na Amboni - Tanga kwa ajili ya taarifa; kupima mipaka katika vituo vya Kalenga na Isimila; kukarabati majengo ya historia ya Caravan Sirai na Ngome Kongwe; kufanya utafiti wa mambo ya kale katika maeneo ya kusini; na kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa malikale.

#### **6.4.4.2. Shirika la Makumbusho ya Taifa**

**207. Mheshimiwa Spika,** Shirika litaratibu Tamasha la Urithi wa Taifa (Urithi festival) litakalofanyika Septemba 2018. Kazi nyingine zitakazofanyika ni kufanya maandalizi ya awali ya kuanzisha Makumbusho ya Marais (*Presidential Museum*) – Dodoma. Aidha, Shirika litaboresha na kuhakikisha usalama wa mikusanyo; litafanya maonesho mawili ya kudumu na manne ya muda; kutangaza Makumbusho na vivutio vyake vya utalii na kufanya Tamasha la Utamaduni wa Mtanzania kwa kushirikisha jamii ya watu wa Mkoa wa Lindi. Vilevile, utafiti utakaowahusisha watafiti wa ndani (3) na watafiti wa nje (10) utafanywa kwenye nyanja 13. Pia, Shirika litafanya kazi za kiushauri na kujenga upya nyumba sita za jadi na utamaduni kwa mpangilio wa ramani ya Tanzania katika Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam.

**208. Mheshimiwa Spika,** Wizara imepanga kupanua Makumbusho ya Elimu Viumbe (*Natural History Museum*) - Arusha ili yajumuishe ukumbi wa Tembo. Hatua hiyo inalenga kuendeleza elimu kuhusu tembo. Makumbusho ya tembo itaonesha chimbuko, maisha na tabia ya tembo. Katika makumbusho hayo, kutakuwa na vioneshwa mbalimbali vinavyohusiana na tembo na maisha yake.

## 6.5. Miradi ya Maendeleo

**209. Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2018/2019 Wizara itatumia jumla ya **Shilingi 29,978,082,000** kutekeleza miradi **11** ya Maendeleo. Fedha hizo zinajumuisha **Shilingi 3,000,000,000** fedha za ndani na **Shilingi 26,978,082,000** fedha za nje. Miradi itakayotekelezwa ni:

- (i) Mradi wa Kusimamia Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini (Resilient Natural Resources for Tourism and Growth - REGROW);
- (ii) Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ikolojia ya Ardhievu ya Bonde la Mto Kilombero na Mto Rufiji (Kilombero and Lower Rufiji Wetlands Ecosystem Management Project - KILORWEMP);
- (iii) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi ya Ujangili (Capacity Building in Game Reserves and Anti-Poaching Unit in Tanzania);
- (iv) Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili (Sustainable Natural Resources Management in Tanzania);
- (v) Mradi wa Misitu Asilia (Enhancing the Forest Nature Reserves Network for Biodiversity Conservation in Tanzania);
- (vi) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Jamii katika Kusimamia Raslimali za Misitu kwa Tija na Misingi Endelevu (Empowering communities through training on participatory forest management, REDD & Climate Change Initiative Program - CCIP);
- (vii) Mradi wa Panda Miti Kibiashara (Support to Private Forest Plantations and Value Chains in Tanzania – PFP);
- (viii) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki (Capacity Building in Forestry and Beekeeping);
- (ix) Mradi wa Kuwezesha Wananchi Kunufaika na Raslimali za Misitu kwa Maendeleo ya Kiuchumi (Natural Resources Management for Local Economic Development - NRM/LED);
- (x) Mradi wa “Theme Park”; na
- (xi) Mradi wa Utalii House Phase II.

Maelezo ya kila mradi yamefafanuliwa kwenye **Jedwali Na. 4**.

## **6.6. Masuala Mtambuka**

### **6.6.1. Utawala na Raslimaliwatu**

**210. Mheshimiwa Spika**, Wizara na Taasisi zake itaendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi wa maliasili, malikale na kuendeleza utalii. Aidha, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwawezesha kupata mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Vilevile, Wizara itaendelea kuongeza na kuimarisha vitendea kazi na kuboresha mazingira ya kazi, na kuhakikisha Wizara inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia misingi ya utawala bora. Pia, Wizara itakamilisha zoezi la kuhamia Dodoma kwa kuhamisha watumishi 46 waliobakia Ofisi ya Dar es Salaam.

### **6.6.2. Kuanzisha Jeshi Usu**

**211. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kukamilisha maandalizi ya kuanzisha Jeshi Usu (Paramilitary) kwa kutoa mafunzo kwa watumishi wa taaluma za wanyamapori, misitu na nyuki; na kujenga uwezo kitaasisi kwa kuongeza vitendea kazi na matumizi ya teknolojia.

### **6.6.3. Mifumo na Matumizi ya TEHAMA**

**212. Mheshimiwa Spika**, Wizara itafanya tathmini ya miundombinu ya TEHAMA ya ndani katika vituo vyote vya kutolea huduma vilivyoko kwenye Wizara na Taasisi zake. Tathmini hiyo itahusisha kuangalia hali ya Mtandao Kiambo (LAN), nguvu ya Nishati, uwezo wa kompyuta, namna bora ya kuvifikia kwa mawasiliano vituo vyote vya maliasili na utalii, na viambatanishi muhimu kwa matumizi ya mfumo wa MNRT Portal. Aidha, miundombinu ya TEHAMA itaanza kufungwa kwenye vituo kulingana na mahitaji.

#### **6.6.4. Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa**

**213. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kutekeleza Mikataba mbalimbali ya ushirikiano ya kikanda na Kimataifa kwenye Nyanja za maliasili, malikale, na utalii ambayo nchi imeridhia.

#### **6.6.5. Kutatua Migogoro**

**214. Mheshimiwa Spika,** Katika kutatua migogoro, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kutatua migogoro kwa kuweka mipaka na vigingi kwenye maeneo ya Hifadhi za wanyamapori, misitu, na malikale; itajenga vituo vya askari kwenye maeneo ya matukio ya mara kwa mara ya wanyamapori wakali na waharibifu; kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi, kuhimiza matumizi ya teknolojia, na kuwekeza katika biashara ya utalii kama njia mbadala ya kipato.

#### **6.6.6. Majukumu ya Kimkakati**

**215. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yake ili kufanikisha mradi wa kuzalisha umeme Rufiji na kuwezesha mazingira ya biashara na uwekezaji. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza maagizo ya viongozi wa Kitaifa yatakayotolewa wakati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti.

### **7.0 SHUKRANI**

**216. Mheshimiwa Spika,** Kipekee napenda kushukuru nchi, mashirika, taasisi na wadau mbalimbali kwa ushirikiano waliotoa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Nachukua fursa hii kutaja baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za China, Denmark, Finland, Hispania, Kanada, Marekani, Norway, Ubelgiji, Ufaransa, Ujerumani, Uswisi na Jumuiya ya nchi za Ulaya. Mashirika na Taasisi ni pamoja na NORAD, AFB, ASEP, EAC, WB, UNDP, SADC, UNESCO, WWF, UNWTO, ICOM, ICCROM, ICOMOS, CITES, USAID, KfW, GIZ, LATF na PAMS Foundation.

## **8.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

**217. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2018/2019, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe jumla ya **Shilingi 115,794,740,000** kwa matumizi ya Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 85,816,658,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 29,978,082,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**218. Mheshimiwa Spika**, Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi 47,758,514,000** za Mishahara na **Shilingi 38,058,144,000** za Matumizi Mengineyo. Aidha, Fedha za maendeleo zinajumuisha **Shilingi 3,000,000,000** fedha za ndani na **Shilingi 26,978,082,000** fedha za nje.

## **9.0 HITIMISHO**

**219. Mheshimiwa Spika**, Ninaomba kuhitimisha kwa kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii itapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii - **[www.mnrt.go.tz](http://www.mnrt.go.tz)**

**220. Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa hoja.

## VIAMBATISHO

**Jedwali Na. 1: Makusanyo ya Maduhuli ya Idara, Taasisi na Mifuko ya Wizara kwa Mwaka 2016/2017, Makisio na Makusanyo hadi Machi 2018, na Makadirio kwa Mwaka 2018/2019**

Idara/Taasisi/ Mifuko	Makusanyo Halisi 2016/17 (Sh.)	Makisio na Makusanyo hadi Machi 2018			2018/2019 (Makadirio) (Sh.)
		Makisio (Sh.)	Makusanyo Julai 2017 hadi Machi 2018 (Sh.)	Asilimia (%)	
(i)	(ii)	(iii)	(iv)	(v)	(vi)
<b>I. Idara</b>					
Utawala na Raslimali Watu	13,717,864	13,004,000.00	4,327,839	33	3,502,126
Utalii	6,770,741,057	20,451,279,008	12,742,851,898	62	22,427,612,375
Wanyamapori	335,964,009	-	12,000,000	100	-
Mambo ya Kale (NAF)	571,000,000	825,000,000.00	916,712,804	111	1,200,000,000
<b>Jumla Ndogo I</b>	<b>7,691,422,930</b>	<b>21,289,283,008</b>	<b>13,675,892,541</b>	<b>64</b>	<b>23,631,114,501</b>
<b>II. Taasisi zilizo chini ya Wizara</b>					
TAWIRI	3,204,224,945	1,419,551,000	840,753,188	59	1,237,730,000
CAWM – Mweka	6,398,164,000	7,659,520,555	3,046,853,748	40	6,463,032,085
PASIANSI	1,560,185,180	1,615,200,000	2,245,515,582	139	2,553,143,000
CBCTC	60,320,000	156,000,000	246,927,770	158	231,000,000
TAFORI	1,093,804,030	431,851,000	811,887,482.40	188	975,000,000
FTI –Olmotonyi	1,295,875,566	3,475,105,000	839,360,740.87	24	4,579,908,160
BTI	150,411,700	291,715,000	375,162,969	129	305,365,000
FITI	158,532,981	606,562,000	247,221,721.95	41	256,000,000
TTSA	1,754,040,808	3,330,600,000	875,703,884	26	4,231,850,000
TTB	636,650,000	2,047,137,000	663,085,994.15	32	640,000,000
NCTA	1,442,305,472	1,887,205,000	1,130,354,216	60	2,553,474,600
NMT	680,000,000	651,000,000	310,818,182	48	700,737,228
<b>Jumla Ndogo II</b>	<b>18,434,514,682</b>	<b>23,571,446,555</b>	<b>11,633,645,478</b>	<b>49</b>	<b>24,727,240,073</b>
<b>III. Mifuko</b>					
TWPF	6,359,132,982	14,600,000,000	3,127,513,675	21	9,200,000,000
TaFF	5,560,228,486	4,117,833,000	3,587,684,378	87	5,618,100,000
<b>Jumla Ndogo III</b>	<b>11,919,361,468</b>	<b>18,717,833,000</b>	<b>6,715,198,053</b>	<b>36</b>	<b>14,818,100,000</b>
<b>JUMLA KUU (I, II &amp; III)</b>	<b>38,045,299,080</b>	<b>63,578,562,563</b>	<b>32,024,736,072</b>	<b>50</b>	<b>63,176,454,574</b>

**Jedwali Na. 2: Makusanyo ya Maduhuli ya Mashirika ya Wizara kwa mwaka 2016/2017, Makisio na Makusanyo hadi Machi 2018, na Makadirio kwa mwaka 2018/2019**

Mashirika	Makusanyo Halisi 2016/2017 (Sh.)	Mwaka 2017/2018			2018/2019 (Makadirio) (Sh.)
		Makisio (Sh.)	Makusanyo Julai 2017 Hadi Machi. 2018 (Sh.)	Asilimia (%)	
(i)	(ii)	(iii)	(iv)	(v)	(vi)
TANAPA	207,523,240,703	205,146,551,383	214,486,751,736	105	292,823,172,000
NCAA	104,080,561,695	88,329,506,000	104,303,346,874	118	156,600,000,000
TAWA	46,936,872,001	44,264,848,333	35,354,464,710	80	47,490,941,150
TFS	102,394,206,890	118,353,938,000	75,935,284,399	64	126,607,334,395
<b>JUMLA</b>	<b>460,934,881,289</b>	<b>456,094,843,716</b>	<b>430,079,847,719</b>	<b>94</b>	<b>623,521,447,545</b>

**Jedwali Na. 3: Mgawanyo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida (Halisi) kwa Idara, Vitengo na Taasisi za Wizara kwa Mwaka 2016/2017, Bajeti na Matumizi hadi Machi 2018 na Makisio kwa Mwaka 2018/2019**

Idara/Kitengo/ Taasisi	Matumizi ya Kawaida (Halisi) 2016/2017 (Sh.)	Bajeti ya Mwaka 2017/2018 (Sh.)			Matumizi Julai 2017 Hadi Machi, 2018 (Sh.)	%	Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka 2018/2019 (Sh.)
		Mishahara	Matumizi Mengineyo	Jumla			
(1)	(2)	(3)	(4)	(5)=(3)+(4)	(6)	(7)=6/5*100	(8)
<b>I: Idara/Kitengo</b>							
Utawala na Raslimaliwatu	4,257,373,956	2,189,826,840	3,368,165,564	5,557,992,404	4,197,942,900	76	5,346,504,496
Fedha na Uhasibu	4,852,096,478	890,218,000	1,000,735,862	1,890,953,862	853,511,729	45	1,494,670,000
Sera na Mipango	721,238,601	329,031,467	1,050,862,048	1,379,893,515	820,917,147	59	1,558,878,048
Mawasiliano	121,206,401	58,520,000	246,211,861	304,731,861	79,228,564	26	368,895,861
Ukaguzi wa Ndani	221,892,001	156,360,000	295,313,837	451,673,837	151,328,195	34	478,477,837
Ugavi	438,469,679	284,724,000	227,411,361	512,135,361	76,540,699	15	628,179,361
Sheria	289,670,319	192,960,000	201,384,000	394,344,000	58,010,050	15	409,524,000
Mifumo ya Kompyuta	116,077,181	109,440,000	440,044,273	549,484,273	157,615,894	29	642,210,451
Wanyamapori	13,962,482,600	13,537,931,333	1,988,893,291	15,526,824,624	8,984,554,174	58	14,805,987,624
Misitu na Nyuki	1,523,999,164	1,975,546,667	593,809,974	2,569,356,641	2,950,250,740	115	2,504,618,049
Utalii	1,749,559,708	815,278,360	2,260,524,340	3,075,802,700	1,565,632,163	51	3,163,323,048
Mambo ya Kale	1,377,470,865	859,189,333	1,341,181,832	2,200,371,165	1,513,192,986	69	2,166,403,118
<b>Jumla Ndogo</b>	<b>29,631,536,953</b>	<b>21,399,026,000</b>	<b>13,014,538,243</b>	<b>34,413,564,243</b>	<b>21,408,725,240</b>	<b>62</b>	<b>33,567,671,893</b>
<b>II: Taasisi/Wakala</b>							
TAWIRI	2,309,191,594	2,174,862,000	78,871,107	2,253,733,107	1,922,011,241	85	2,238,192,282
CAWM (MWEKA)	2,206,817,379	2,060,640,000	150,958,495	2,211,598,495	1,456,913,064	66	2,133,785,794
Likuyu Sekamaganga	118,743,517	0	110,849,649	110,849,649	53,574,600	48	110,123,672
Pasiansi	132,123,392	0	129,308,955	129,308,955	75,776,800	59	128,462,033
TAWA	563,820,750	0	1,401,974,258	1,401,974,258	619,204,300	44	1,784,373,595
TAFORI	2,370,866,354	2,063,892,000	281,821,361	2,345,713,361	1,680,696,350	72	2,240,511,405
FITI	221,544,054	0	257,108,055	257,108,055	141,411,600	55	255,424,550
FTI	267,712,029	0	192,088,942	192,088,942	105,646,200	55	190,831,260
BTI	172,184,924	0	177,321,601	177,321,601	142,528,200	80	176,160,669
TFS	15,045,849,295	26,457,474,000	19,462,289,042	45,919,763,042	11,041,537,572	24	36,143,832,214
TTSA	537,870,441	0	586,512,000	586,512,000	417,407,200	71	665,130,000
NCTA	1,674,249,083	1,156,296,000	618,752,151	1,775,048,151	1,152,779,756	65	1,720,272,062
TTB	4,488,035,533	1,048,561,000	2,408,062,566	3,456,623,566	2,285,613,995	66	2,475,411,294
NMT	2,172,998,206	1,625,424,000	355,236,784	1,980,660,784	1,399,991,597	71	1,986,475,277
<b>Jumla Ndogo</b>	<b>32,282,006,551</b>	<b>36,587,149,000</b>	<b>26,211,154,966</b>	<b>62,798,303,966</b>	<b>22,495,092,475</b>	<b>36</b>	<b>52,248,986,107</b>
<b>JUMLA KUU (I+II)</b>	<b>59,263,073,902</b>	<b>57,986,174,997</b>	<b>39,225,693,205</b>	<b>97,211,868,209</b>	<b>44,990,184,950</b>	<b>46</b>	<b>85,816,658,000</b>

**Jedwali Na. 4: Makadirio ya Matumizi kwa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2018/2019**

Na. Kifungu	Na. ya Mradi	Jina la Mradi	Eneo la Mradi	2018/2019		Jumla (Sh.)	Mhisani
				Fedha za Ndani (Sh.)	Fedha za Nje (Sh.)		
(i)	(ii)	(iii)	(iv)	(v)	(vi)	(vii)	(viii)
<b>1003</b>	<b>Idara ya Sera na Mipango</b>						
1	5203	Resources Management for Tourism and Growth Project (REGROW)	Hifadhi za Taifa za Ruaha, Udzungwa, Mikumi na Pori la Akiba Selous.	500,000,000	2,751,120,000	3,251,120,000	World Bank/GoT
<b>Jumla Ndogo</b>				<b>500,000,000</b>	<b>2,751,120,000</b>	<b>3,251,120,000</b>	
<b>2001</b>	<b>Idara ya Wanyamapori</b>						
2	4809	Kilombero and Lower Rufiji Wetland Management Project	Wilaya za Rufiji, Ulanga, Kilombero na Malinyi.	0	1,494,193,471	1,494,193,471	Belgium
3	4810	Capacity Building in Game Reserves and Anti-poaching Unit in Tanzania	Mapori ya Akiba ya Burigi, Biharamulo na Kimisi.	1,000,000,000	0	1,000,000,000	GoT
4	4811	Sustainable Natural Resources Management in Tanzania	Hifadhi ya Taifa Serengeti, Pori la Akiba Selous, Pori Tengefu la Loliondo na Maeneo ya wazi yanayozunguka hifadhi hizo.	0	11,969,405,536	11,969,405,536	German
<b>Jumla Ndogo (Wanyamapori)</b>				<b>1,000,000,000</b>	<b>13,463,599,007</b>	<b>14,463,599,007</b>	
<b>3001</b>	<b>Misitu na Nyuki</b>						
5	4631	Enhancing the Forest Nature Reserves Network for Biodiversity Conservation in Tanzania	Misitu ya Hifadhi ya Mazingira Asilia Chome, Magamba, Mkingu, Minziro, Udzungwa na Rungwe.	0	1,364,097,000	1,364,097,000	UNDP/GEF
6	4646	Participatory Forest Management, REDD and	Chuo cha Misitu Olmotonyi.	0	757,825.000	757,825.000	Norway

Na. Kifungu	Na. ya Mradi	Jina la Mradi	Eneo la Mradi	2018/2019		Jumla (Sh.)	Mhisani
				Fedha za Ndani (Sh.)	Fedha za Nje (Sh.)		
(i)	(ii)	(iii)	(iv)	(v)	(vi)	(vii)	(viii)
		CCIP					
7	4647	Private Plantation Forestry and Value Chain in Tanzania	Wilaya za Njombe, Makete, Kilolo, Mufindi na Kilombero.	0	5,950,860,993	5,950,860,993	Finland
8	4648	Capacity Building in Forestry and Beekeeping Training Institutes in Tanzania	Chuo cha Mafunzo ya Nyuki Tabora, Chuo cha Misitu Olmotonyi, Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi na Njiro - TAWIRI.	500,000,000	0	500,000,000	GoT
9	4649	Natural Resources Management (LED)	Wilaya za Uvinza, Kakonko, Kasulu, Kigoma, Kibondo na Buhigwe.	0	2,690,580,000	2,690,580,000	Belgium
		<b>Jumla Ndogo</b>		<b>500,000,000</b>	<b>10,763,362,993</b>	<b>11,263,362,993</b>	
<b>4001</b>		<b>Idara ya Utalii</b>					
10	5202	Construction of Theme Park in Dar es Salaam City	Jiji la Dar es Salaam	500,000,000	0	500,000,000	GoT
11	6367	Utalii House Phase II	Jiji la Dar es Salaam	500,000,000	0	500,000,000	GoT
		<b>Jumla Ndogo</b>		<b>1,000,000,000</b>	<b>0</b>	<b>1,000,000,000</b>	
		<b>Jumla Kuu</b>		<b>3,000,000,000</b>	<b>26,978,082,000</b>	<b>29,978,082,000</b>	

**Jedwali Na. 5: Idadi ya Watalii wa Ndani na Nje Waliotembelea Hifadhi za Taifa na Mapato yaliyopatikana kuanzia 2013/2014 hadi Machi 2018**

Mwaka wa Fedha	Watalii wa Nje	Watalii wa Ndani	Jumla ya Watalii	Mapato (Sh.)
2013/2014	530,142	427,208	957,350	150,861,426,031
2014/2015	526,110	432,124	958,234	149,957,485,000
2015/2016	518,457	439,119	957,576	175,089,696,000
2016/2017	595,811	386,529	982,340	207,587,218,000
2017/2018*	564,418	331,576	895,994	214,486,751,736

\*Hadi Machi 2018

**Jedwali Na. 6: Idadi ya Watalii wa Ndani na Nje Waliotembelea Mamlaka ya Ngorongoro na Mapato yaliyopatikana kuanzia 2013/2014 hadi Machi, 2018**

Mwaka wa Fedha	Watalii wa Nje	Watalii wa Ndani	Jumla ya Watalii	Mapato (Sh.)
2013/2014	341,779	281,663	623,442	61,664,100,836
2014/2015	311,814	281,637	623,442	60,687,703,795
2015/2016	291,525	297,856	1,246,884	70,705,588,376
2016/2017	352,991	248,224	2,493,768	102,128,858,941
2017/2018*	337,920	188,043	4,987,536	104,303,346,874

\*Hadi Machi 2018

**Jedwali Na. 7: Mapato kutokana na Uwindaji wa Kitalii kuanzia Mwaka 2015 hadi 2017**

Mwaka	Idadi ya Watalii			Mapato (Sh.)
	Wawindaji	Watazamaji (Observers)	Jumla	
2015	608	393	1001	28,802,391,200
2016	495	297	792	29,136,885,800
2017	473	291	764	19,202,957,607

**Jedwali Na. 8: Mwenendo wa Upandaji miti katika Mashamba ya Miti nchini kwa Mwaka 2013/2014 hadi Machi, 2018**

<b>Shamba</b>	<b>2013/14</b>	<b>2014/15</b>	<b>2015/16</b>	<b>2016/17</b>	<b>2017/18*</b>	<b>Jumla (ha)</b>
Buhindi	289.00	561.90	794.69	559.00	771.28	2975.87
Kawetire	294.00	460.20	485.50	174.00	263	1676.7
Kiwira	95.00	123.00	111.50	132.00	62	523.5
Korogwe	-	70.00	250.00	12.00	64	396
Longuza	50.00	109.50	43.50	40.00	41	284
Mbizi	168.00	538.80	520.00	480.00	218	1924.8
Meru-USA	344.37	210.62	129.00	36.80	291	1011.79
Mtibwa	264.00	300.00	276.60	-	516	1356.6
Morogoro	-	-	42.50	42.50	45	130
North Kilimanjaro	213.00	221.0	204.70	115.00	3	756.7
North Ruvu	-	73	250	225	81	629
Biharamulo	-	-	-	-	446	446
Mpepo	-	-	-	-	200	200
Iyondo Msimwa	-	-	-	-	220	220
Buhigwe	-	-	-	-	100	100
Rondo	114.40	118.10	205.20	251.00	196	884.7
Rubare	380.00	500.00	380.00	414.00	104	1778
Rubya	36.00	21.00	271.60	150.00	203	681.6
Sao Hill	5,072.94	3,655.20	3,421.98	4,050.00	2,399	18,599.12
Shume	381.06	149.00	103.30	75.70	168	877.06
Ukaguru	180.00	160.00	207.00	270	230	1047
West Kilimanjaro	45.60	142.00	130.20	152.68	62	532.48
Winno-Ifinga	500.00	747.60	733.00	678.00	883.2	3541.8
<b>Jumla (hektari)</b>	<b>8427.37</b>	<b>8160.92</b>	<b>8560.27</b>	<b>7857.68</b>	<b>7566.48</b>	<b>40572.72</b>

\*Hadi Machi, 2018

**Jedwali Na. 9: Mauzo ya Asali na Nta Ndani na Nje ya Nchi kwa Mwaka 2010/2011 – 2016/2017**

Mwaka wa Fedha	Mauzo (Tani)				Uzalishaji (Tani)	
	Ndani ya Nchi		Nje ya Nchi		Asali	Nta
	Asali	Nta	Asali	Nta		
2010/2011	800.38	59.33	343.02	534	1,143.40	593.33
2011/2012	486.54	46.49	208.516	418.369	695.05	464.85
2012/2013	217.16	26.81	93.068	241.3	310.23	268.11
2013/2014	295.63	46.93	126.7	422.41	422.33	469.34
2014/2015	356.07	24.47	152.6	220.22	508.67	244.69
2015/2016	606.34	27.99	259.86	251.93	866.20	279.92
2016/2017	439.97	22.65	188.56	203.85	628.53	226.50

**Jedwali Na. 10: Mwenendo wa Biashara ya Utalii Nchini 2013-2017**

Mwaka		2013	2014	2015	2016	2017
Idadi ya watalii		1,095,884	1,140,156	1,137,182	1,284,279	1,327,143
Idadi ya watalii hotelini		1,021,766	1,054,338	1,033,555	1,145,934	1,163,752
Mapato (US \$ million)		1,853.28	2,006.32	1,901.94	2,131.57	2,250.3
Wastani wa siku za kukaa watalii hotelini		10	10	10	10	10
Wastani wa matumizi ya fedha kwa mtalii kwa siku (US \$)	<i>Package Tour</i>	372	277	305	290	411
	<i>Non Package Tour</i>	201	117	141	131	136

**Jedwali Na. 11: Idadi ya Wageni Waliotembelea Vituo vya Mambo ya Kale na Mapato yaliyopatikana kwa Kipindi cha 2013/2014 hadi Machi, 2018**

KITUO	2013/2014		2014/2015		2015/2016		2016/2017		2017/2018*	
	Wageni	Mapato (Sh.)	Wageni	Mapato (Sh.)						
Bonde la Olduvai	42,557	995,615,000	39,716	832,881,000	-	383,953,250	-	669,272,255	34,724	2,093,373,590
Magofu ya Kaole	46,102	40,000,000	38,536	42,293,000	13,967	36,503,000	12,328	25,809,000	10,458	27,242,000
Zama za Mawe Isimila	4,443	9,513,500	4,766	11,595,000	2,030	11,970,000	1,870	8,617,000	1,445	8,167,000
Mji Mkongwe, Bagamoyo	14,484	13,913,000	11,707	16,741,500	7,515	26,902,000	10,931	23,989,500	6,798	24,324,000
Kaburi la Mtwaa Mkwawa, Kalenga	2,170	5,261,000	2,956	3,914,000	1,048	2,533,000	1,105	1,523,500	1,501	2,105,000
Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara	2,209	16,611,400	3,330	18,362,500	2,366	21,631,000	2,274	15,411,000	1,083	10,439,000
Kimondo cha Mbozi	893	1,361,000	1,681	2,426,000	1,476	3,030,000	1,164	2,046,000	1,368	3,039,000
Mapango ya Amboni	27,073	26,015,000	27,687	26,973,000	11,755	23,157,500	6,005	11,549,000	21,662	19,377,000
Magofu ya Tongoni	397	898,200	829	873,000	369	1,695,000	293	1,331,000	104	792,000
Dkt. Livingstone Ujiji, Kigoma	4,937	9,411,300	5,020	9,543,200	3601	9,655,000	2,522	5,680,000	2,606	6,224,000
Tembe la Kwihara	428	495,000	282	380,000	431	899,500	238	520,000	361	902,000
Michoro ya Miambani Kondoa, Kolo	1,239	6,844,500	1,216	8,578,000	2,027	9,204,000	881	6,696,000	1,766	12,550,000
Makumbusho ya Caravan Serai, Bagamoyo	8,095	7,499,000	9,324	10,319,700	3,155	9,143,000	3,537	7,174,500	1,814	4,246,000
Magomeni	-	-	-	-	-	-	149	274,500	302	608,000
<b>JUMLA KUU</b>										
									<b>85,992</b>	<b>2,213,388,590</b>

\*Hadi Machi, 2018

**Jedwali Na. 12: Takwimu za Wageni Waliotembelea Makumbusho ya Taifa na Mapato kwa mwaka 2015/2016 hadi Machi, 2018**

KITUO/ MAKUMBUSHO	2015/2016				2016/2017				2017/2018*			
	Wageni			Mapato (Sh.)	Wageni			Mapato (Sh.)	Wageni			Mapato (Sh.)
	Nje	Ndani	Jumla		Nje	Ndani	Jumla		Nje	Ndani	Jumla	
Nyumba ya Utamaduni	8,398	22,385	30,782	319,489,412	7,429	17,114	24,543	417,038,063	6,908	11,272	18,180	174,357,716
Kijiji cha Makumbusho	3,578	41,971	45,550	60,336,694	3,092	40,523	43,615	78,759,098	4,271	35,809	40,080	55,357,716
Azimio la Arusha	325	19,333	19,658	27,615,600	1839	7,897	9,736	36,047,380	356	7,766	8,122	9,773,633
Elimu Viumbe	1,199	9,166	10,364	44,003,400	1,750	5,199	6,950	57,438,813	3,726	7,313	11,039	59,219,468
Mwl. J.K. Nyerere	1078	9,013	10,091	5,555,040	73	8,036	8,110	7,251,142	627	8,587	9,214	5,876,239
Vita vya Majimaji	78	6,044	6,122	4,715,400	82	7,158	7,240	6,155,138	154	5,998	6,152	5,630,655
<b>Jumla</b>	<b>14,656</b>	<b>107,912</b>	<b>122,568</b>	<b>461,715,546</b>	<b>14,266</b>	<b>85,927</b>	<b>100,193</b>	<b>602,689,634</b>	<b>16,042</b>	<b>76,745</b>	<b>92,787</b>	<b>310,818,182</b>

\*Hadi Machi, 2018

**Jedwali Na. 13: Mapato Yatokanayo na Vibali vya Utafiti wa Raslimali za Malikale na Utafutaji wa Tunu kwa Mwaka 2013/2014 hadi Machi, 2018**

Mwaka	Mapato (Sh.)		
	Utafiti wa kisayansi	Utafiti wa Tunu	Jumla
2013/2014	7,002,280	1,195,750	<b>8,198,030</b>
2014/2015	37,473,674	2,850,775	<b>40,324,449</b>
2015/2016	13,240,710	5,923,825	<b>19,164,535</b>
2016/2017	20,580,456.50	3,320,225	<b>23,900,681.50</b>
2017/2018*	10,992,964.47	5,456,030	<b>16,448,994.47</b>

\*Hadi Machi, 2018

**Jedwali Na. 14: Idadi ya Wanafunzi Waliodahiliwa katika Vyuo vya Wizara katika Kipindi cha 2013/2014 hadi 2017/2018**

Chuo	Wanyamapori			Utalii	Misitu na Nyuki			Jumla
	Mwaka	Pasiansi	Likuyu Seka-maganga		NCT	FITI-Moshi	BTI-Tabora	
2013/2014	540	400	189	242	32	40	167	<b>1,610</b>
2014/2015	616	415	83	218	30	79	266	<b>1,707</b>
2015/2016	578	441	91	201	73	91	519	<b>1,994</b>
2016/2017	560	441	100	315	100	150	450	<b>2,116</b>
2017/2018	551	441	97	228	133	201	672	<b>2,323</b>